# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 30, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581723

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UCHAGUZI 2024, 2025

**TAKUKURU** yasuka mkakati kunasa wanaoendekeza vitendo vya rushwa

UKURASA 8



MAISHA YALIVYO

**Mke** akitoa siri za ndani jitafakari!

UKURASA 11



**Muda** waongezwa Kliniki ya Makonda matibabu ya bure

UKURASA 2

UKURASA 20

**Tanasha akubali matokeo**



RIPOTI MAALUM

# Undani wa ajali zinazoua ndugu kwa pamoja

• **Wasaikolojia** tiba, polisi wafichua mazito... *Endelea ukurasa 4*

UKURASA WA 17

## WANAJESHI KUENDELEA KUILINDA MITAA KENYA



SERIKALI ya Kenya, imesema jeshi la nchi hiyo litaendelea kushika doria mitaani hadi hali ya kawaida itakaporejea.

## Mjumbe NEC: Kuna kundi linaichafua CCM

UKURASA 3



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akihutubia wananchi wa Kikunde, Kilindi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe acharuka saruji kupanda bei UK. 2

**MICHEZO** **SIMBA YAIFUNIKA ORLANDO PIRATES** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Mbowe ageukia upandaji bei ya saruji

**Na Godfrey Mushi,** KITETO

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema kupanda kwa bei ya saruji katika maeneo mbalimbali nchini kunatokana na kodi iliyowekwa na serikali katika bidhaa hiyo ambayo ni kati ya Sh. 7,000 hadi 9,000.

Akizungumza jana na wananchi wa Matui, wilayani Kiteto, mkoani Manyara katika mwendelezo wa mikutano ya 'Operesheni GF', Mbowe alisema katika kila mfuko mmoja wa saruji, serikali inaweka kodi hiyo.

"Mfuko mmoja wa saruji watu wa Matui (Kiteto), mnanunua kwa shilingi ngapi? 20,000/- Kwa taarifa yenu, kwenye kila mfuko mmoja wa cement (saruji), serikali ya CCM inaweka kodi kati ya Sh. 7,000 na 9,000.

"Matokeo yake, ukienda kununua mfuko wa saruji Sh. 20,000 au Sh. 21,000, tayari umeshalipa kodi ya serikali ya CCM. Kila kitu mnachonunua kina kodi ya serikali.

Aliwaeleza kwamba wakienda kununua mabati, muda wa maongezi katika simu, umeme, mafuta ya taa, mafuta ya kupikia, sabuni au soda kote kuna kodi.

Mbowe alisema bidhaa za vinywaji kama soda, kiwandani ni Sh. 270, lakini katika kila chupa moja ya soda serikali imeweka kodi Sh. 230, hivyo ikimfikia mwananchi haipungui Sh. 600.

"Ndugu zangu kama tuna shida ya elimu bora tuna shida wote, kama tuna shida ya maji, tuna shida wote. Kama tuna gharama za maisha, wote tuna gharama za maisha. Sasa unakuta wananchi wa Matui hawana maji, yuko hoi, hajitambui sawasawa," alisema.

Mbowe na Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, wanazunguka katika majimbo 35 ya mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga kwa wiki tatu mfululizo, wakiendesha Operesheni GF.




Ujenzi wa Barabara ya Nyerere ukiendelea eneo la Daraja la Chang'ombe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kliniki ya Makonda yaongezwa muda

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

KUTOKANA na wingi wa wananchi kuendelea kujitokeza katika kambi ya matibabu mkoani Arusha, serikali imeongeza muda wa siku moja ili kila aliyejitokeza apatiwe huduma.

Vilevile, watu 700 waliobainika kuwa na shida kubwa kiafya, watatibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa gharama za serikali.

Hayo yalisemwa jana mkoani Arusha na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alipozungumza na wananchi waliojitokeza kwenye kambi hiyo kupatiwa matibabu bila malipo iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda.

Alisema kinachofanyika katika kambi hiyo ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwa amezunguka nchini na kujifunza kwamba kuna Watanzania wengi ambao wanahitaji huduma za madaktari bingwa wabobezi lakini hawawezi kuzipata.

Naibu Waziri Mollel alisema kuna wengine wanakosa hata nauli ya kufika katika hizo hospitali kubwa.

"Wengine wanaweza kupata nauli lakini uwezo wa kujihudumia hawana, hivyo Rais alitoa maelekezo watoke na kushuka chini kuwafuata wananchi waliko," alisema.

Dk. Mollel alisema katika kambi hiyo wapo wananchi waliotokea katika mikoa mbalimbali, wamefika katika kambi hiyo ya matibabu ili kutibiwa.

"Wapo wananchi waliotoka mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Kilimanjaro na wengine hadi wametokea Mbeya, maana yake pamefanyika hamasa nzuri ya kujua madakatri bingwa wabobezi wapo Arusha na hili tumpongeze Makonda," alisema.

Dk. Mollel alisema hiyo ni programu maalum ya kibingwa ya Rais Samia na tayari amesaidia kuwezesha kila huduma kupatikana bure kwa wananchi.

Alisema kuwa hadi juzi, jumla ya wananchi 28,976 wametibiwa na wale ambao wanatakiwa kwenda MNH ni 700 na watakaopelekwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wapo 200, watatibiwa kupitia programu hiyo ya Rais Samia.

"Kwa hapa Mkoa wa Arusha, kwa wale waliotoka wilayani walishindwa kwenda hospitali ya mkoa mpaka juzi waliotibiwa katika Hospitali ya Mount Meru ni 466. Maana yake mpaka Jumatatu tuliyoiongeza wananchi wengi watakuwa wamepata huduma," alisema.

Naibu Waziri alisema wananchi hao 28,976 ambao wametibiwa walishindwa kupata huduma kwa utaratibu wa kawaida, walihitaji kusaidiwa, hivyo wanahitaji kuongeza nguvu katika mkakati wa Rais Samia.

Alisema wanahitaji madaktari wao waendelee kushuka chini zaidi na kuongeza nguvu katika hospitali za wilaya kwa kuwa kuna wagonjwa wengi ambao hawakuhitaji hata kufika katika kambi hiyo, wangetibiwa hukohuko.

"Idadi ya watu inazidi kuongezeka, hawa wote walitakiwa kutoa fedha mfukoni wapate matibabu lakini hawana, wamekuja hapa.

"Katika hii huduma tumepata funzo kuwa inahitajika bima ya afya kwa wote, ni suala la kipaumbele," alisema Naibu Waziri Mollel.

Alisema anakwenda kuongeza idadi ya wafamasia wafike katika eneo hilo ili kupunguza foleni ya utoaji dawa kwa wananchi.

Alisema wataongeza pia madaktari ili kuhakikisha siku mbili zilizobaki wananchi wanapatiwa matibabu kwa wakati na kuondoa msongamano wa watu.

Makonda alisema wamesitisha kutoa namba mpya kwa wagonjwa kutokana na kuwapo idadi kubwa ya watu ambao hawajahudumiwa.

"Tunachoshindwa ni kuendelea kuongeza watu wakati tuliokuwa nao hatujawamaliza kuwahudumia tusingependa kuona hii hali inaendelea hadi Jumatatu, itakuwa haina faida walau tumalize tuliowapa namba ndio maana tumekubaliana kule tusitoe tena namba ili wote mhudumiwe waishe," alisema Makonda.

Makonda alisema tayari kuna wadau wengine jana waliwaletea dawa za Sh. milioni 31 kutoka Samiro Pharmacy Ltd na Benki ya NMB imewapatia dawa za Sh. milioni 10 na gari la kubeba wagonjwa.

Mkuu wa Mkoa huyo aliendelea kuomba wananchi kuzingatia utaratibu uliopangwa badala ya kuharibu foleni ili kila mmoja apatiwe matibabu.

**WIZI WA SIMU**

Wakati wananchi wakiwa kwenye foleni kwa ajili ya kusubiria matibabu, kuna tatizo limeripotiwa la kuibiwa simu zao, jambo lililozua taharuki.

Aliyekuwa akitangaza matangazo uwanjani hapo kila wakati alikuwa akipokea taarifa ya kuibiwa simu na kuwatangazia wananchi.

Alieleza kuwa kuna wimbi kubwa la wizi wa simu unaoendelea kwenye foleni na wananchi kuombwa kuongeza umakini katika kulinda mali zao.

"Kuna wimbi kubwa la wizi wa simu unaoendelea, tunaomba muwe makini siyo wote wapo katika foleni ya ugonjwa,wengine ni wezi. Na wewe unayeiba simu tunakupa dakika 45 tutakukamata," alionya.

ZUIO UVUVI ZIWANI

# Mjumbe NEC: Kuna kundi linaichafua CCM

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Rukwa, Sultan Saleh Seif, ametoa ufafanuzi kuhusu hoja ya kuruhusu wananchi kuvua katika Ziwa Tanganyika ambao serikali imesitisha shughuli za uvuvi kwa miezi mitatu.

Amesema kuna kundi linatumia jina lake kutaka kuichafua CCM kisiasa na hata kumgombanisha yeye binafsi na uongozi wa chama hicho.

Seif alitoa ufafanuzi huo jana alipozungumza na Nipashe Jumapili baada ya kuwapo kipande kifupi cha video kinachosambazwa mitandaoni, kikimnukuu akiruhusu wananchi kuvua katika ziwa hilo.

Serikali imeshatangaza kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kuanzia Mei 15 hadi Agosti 15 mwaka huu.

Seif alisema kuwa kipande cha video kinachosambazwa mitandaoni ni sehemu ya video ndefu iliyorekodiwa Juni 26 mwaka huu wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Ninde, Kata ya Ninde, wilayani Nkasi wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara.

Hata hivyo, Seif alisema kipande hicho kimekatwa kwa ustadi kuonesha anapingana na serikali, akisisitiza hawezi kufanya hivyo, ana njia nyingi za kuikosoa na kuishauri serikali na si katika muktadha wa aina hiyo.

"Ukweli ni kwamba nilikuwa katika mikutano ya kawaida ya chama. Nilipofika katika kijiji hicho (Ninde), kukawa na malalamiko ya wananchi kuhusu kuzuiwa kuvua Ziwa Tanganyika.

"Nikampigia mbunge wetu, nikamweleza 'nipo Kijiji cha Ninde kwenye jimbo lako, nilipofika hapa nimeweleza wananchi waliokusanyika kwamba unahitaji kuwasalimia na umewakumbuka sana... na leo huwezi kulala kama hujawasalimu'.

"Mbunge alisema (kama ilivyo katika video nzima ya mkutano huo) 'nipo bungeni ninaendelea kupambana kwa ajili ya Ninde, ninajua ilivyokuwa hapo kipindi cha uchaguzi mlikuwa hamna barabara, usalama wa Ziwa Tanganyika tunajenga kambi ya jeshi Kata ya Kizumbi, boti zitakuja kwa ajili ya patroo, wavuvi wanatakiwa wavue kwa usalama bila kubugudhiwa na majambazi.

> **Uvuvi wa mabwawani samaki kwaajili ya mboga unaruhusiwa (yowe likatawala) msizuiliwe kuvua samaki kwa ajili ya mboga, rukhsa hiyo ni kwa uvuvi wa ndoani, si kwa wale wanaotumia wavu,**

"Pili, uvuvi wa mabwawani samaki kwaajili ya mboga unaruhusiwa (yowe likatawala) msizuiliwe kuvua samaki kwa ajili ya mboga, rukhsa hiyo ni kwa uvuvi wa ndoani, si kwa wale wanaotumia wavu, uvuvi wa ndoano mtu na familia yake kwenda kuvua pembezoni akale chakula kwa ajili ya mboga ni rukhsa."

Seif anaendelea kueleza kuwa, "Nilimpomwuliza mbunge kwamba baada ya mkutano huo wananchi waende wakavue samaki kwa kutumia ndoano, alijibu 'ndio'."

Kuhusu barua kutoka wizarani ya katazo hilo la uvuvi, mbunge alisema anashughulikia barua ya wizara kuja katika wilaya.

Baada ya maelezo hayo ya mbunge, Seif anasema aliwageukia wananchi, akisema (kama ilivyo katika video nzima) "muwe waadilifu, msiende huko mkavua kwa vitu ambavyo haviruhusiwi na hapa mmemsikia mbunge mwenyewe kasema na amezungumza na waziri, anayetakiwa kutoa rukhsa hii ni mkuu wa wilaya, hapa hayupo anayemwakilisha atamwambia haya ni maelekezo ya chama kwa kuwa hili jambo lipo kisheria."

Hata hivyo, Seif alisema kauli yake hiyo inapotoshwa makusudi kwa lengo la kumwonesha anapingana na maelekezo ya serikali.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akitangaza uamuzi wa serikali kufunga kwa muda shughuli za uvuvi, alisema lengo ni kupumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu ili kuwezesha samaki kuzaliana na kuongeza tija kwa wavuvi wanaofanya shughuli zao ziwani huko.

Ulega alisema uamuzi wa Tanzania unatokana makubaliano yaliyoazimiwa katika kikao kilichofanyika mwaka 2022, kikihusisha nchi zinazozunguka ziwa hilo ambazo ni Zambia, Tanzania, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ulega alisema uamuzi huo ni utekelezaji Mkataba wa Kikanda wa Nchi Wanachama wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika unaoweka hatua na taratibu za usimamizi endelevu wa shughuli za uvuvi katika ziwa hilo.

Waziri huyo aliongeza uamuzi huo unatokana na utafiti uliobainisha kuwa kuna upungufu mkubwa wa samaki na dagaa katika Ziwa Tanganyika kutokana na ongezeko kubwa la uvuvi usio endelevu uliosababisha uharibifu wa mazalia ya samaki.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MAALUM

# Undani ajali zinazoua ndugu wengi pamoja

**Romana Mallya na Godfrey Mushi**

AJALI zinazosababisha vifo vya ndugu wengi kwa wakati mmoja zina madhara makubwa kisaikolojia, wataalamu wamethibisha.

Wameonya kuwa wanaopoteza wapendwa wao kutokana na ajali hizo, wasipopata tiba ya kisaikolojia mapema, wanakuwa katika hatari kupata kiwewe (trauma) na msongo mkubwa wa mawazo, hata kutishia uhai wao.

Ni angalizo linalotolewa na wataalamu hao kipindi ambacho kumekuwa na ajali za barabarani zinazosababisha vifo vya ndugu wanaosafiri pamoja katika maeneo mbalimbali nchini.

Ajali hizo ni pamoja na mwanzoni mwa juma hii (Juni 24) wilayani Korogwe, mkoani Tanga iliyohusisha wanafamilia, wanne wakifariki dunia wakati wakitoka kwenye harusi ya kijana wao jijini Dar es Salaam, wakirejea kwao Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Msaikolojia Tiba kutoka Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Isaac Lema, anasema majonzi kwa wale ambao wamepoteza ndugu kwa wakati mmoja katika ajali huwa hayaelezeki na huchangia wahusika kubaki na maswali yasiyo na majibu.

"Kuna lile swali 'imekuaje?' Huja na kiwango cha juu cha msongo kiasi ambacho wengine katika hilo wanapata kipindi kirefu cha kuwa katika hali ya kutokuwa sawa na wasipopatiwa msaada wa karibu msiba huwa mzito.

"Ndio maana misiba ya namna hii ambayo hujitokeza katika hali isiyotarajiwa, unakuta faraja yake huwa tofauti, kunakuwa na wingi wa watu. Asipopata faraja kubwa au usaidizi wa kutosheleza inatishia pia uhai wake.

"Ikifika mahali ikatishia maisha yake na kutaka kuwa msongo wa juu, linaanza kugeuka kuwa jeraha la kisaikolojia.

"Mara nyingi misiba ya namna hii huleta kiwewe na kusababisha kuona wale watu (ndugu) kama wanajitokeza (mbele yao), hivyo jeraha linakuwa kubwa," Lema anasema.

Msaikolojia Tiba huyo anasema wamekuwa wakipokea watu wa namna hiyo na jambo la kwanza katika kuwatibu, hujielekeza kutambua kiwango chao cha msongo, wameathirika kwa kiwango gani.

"Kama ni jeraha tunatibu, kama litahitaji msaada saidizi tunatoa msaada wa kwanza wa kisaikolojia wa kijamii ambao unawajengea uwezo wa kupambana na hiyo hali mapema. Tunapowaona mapema ndio tunazuia madhara makubwa yasijitokeze.



"Wakifika mapema tunawasaidia kuwakinga dhidi ya magonjwa ya akili ambayo yanaweza kujitokeza, mfano, msongo baada ya janga na wakati huohuo tunatengeneza mazingira ya kumsaidia aliye na jeraha apatiwe matibabu, kwa sababu kuna matibabu ya kisaikolojia ya kutibu majeraha hayo," Lema anafafanua.

Mtaalamu huyo anasema wanapotibiwa majeraha hayo, huwa wanasonga mbele, huku wakiendelea kuwafuatilia kwa kuwa huchukua hadi miezi mitatu, sita na wakati mwingine mwaka mzima kutegemeana na uwezo wa mhusika katika kukabiliana na janga hilo.

"Si lazima akubaliane na hali. Unaweza kukubaliana na hali, lakini hujarudi kwenye hali ya kawaida. Mfano, kama amekubaliana na hali lakini hajaweza kuishi pasipo yule mhusika, bado itakuwa changamoto," Lema anasema.

Msaikolojia huyo anatoa wito kwa wote wanaopata changamoto hizo, wapatiwe huduma mapema ili kukingwa dhidi ya magonjwa ya akili yanayoweza kujitokeza kwa kuwa mengi huwapokea wakiwa na msongo mkubwa.

Jambo la pili, Lema anasema kwa wale walioachwa wanapaswa kujengewa uthabiti ili maisha yao yasonge mbele.

Msaikolojia Tiba huyo anashauri watu waepuke kusafiri ndugu wengi kwa chombo. Panapokuwa na ulazima wa kufanya hivyo, basi kuwe na utii wa sheria za usalama barabarani.

"Ndugu kusafiri katika chombo cha usafiri kimoja huchangiwa na mazingira fulani na wakati mwingine hayawezi kuepukika, hivyo ikitokea hivyo ni muhimu kufuata kanuni na sheria za usalama barabarani na kuvijua vyombo wanavyosafiria vikoje.

"Wapo wengi wanaosafiri katika chombo kimoja kama familia, lakini hawakutani na majanga hayo. Kwanini? Ni kwa sababu wanafuata kanuni na sheria za usalama barabarani, na huwa wanakumbushana mwendo wa familia. Ajali haina kinga, lakini tuna uwezo wa kuzuia isitokee," anasema.

**KIINI CHA AJALI**

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Naibu Kamishna wa Polisi Ramadhan Ng'azi, anatoa wito kwa familia wanaposafiri pamoja kuwa waangalifu barabarani.

"Tumezoea kuona wakati wa sikukuu mwishoni mwa mwaka au katika matukio ya kijamii yanayopelekea wanafamilia husafiri chombo kimoja, kwa kuwa wanakuwa wanafahamiana umakini barabarani mara nyingi hupungua.

"Unakuta wanapita hoteli mbalimbali wanapata chakula au vinywaji vinavyowaondolea umakini barabarani hasa safari ndefu wanaona ni sehemu ya kufurahi na kunywa bia.

"Wito wetu ni huu; siku zote watu wanapokuwa safarini iwe wanafamilia au wengine, umakini uongezwe kwa kuzingatia kwamba katika safari za familia kama dereva ni mmoja wawe makini.

"Unakuta mtu hajawahi kusafiri umbali mrefu, mfano Dar-Bukoba au Dar-Mbeya, Dar-Arusha au Dar-Manyara, uchovu unakuwa mwingi.

"Amezoea Kimara-Posta, hivyo kwa umbali mrefu anakuwa hana uzoefu, lakini hapohapo anakunywa vinywaji ambavyo haviruhusiwi au vyakula ambavyo vitamfanya kusinzia," anasema.

Kamanda Ng'azi anasema mara nyingi ajali hizo hutokea kwa sababu za uchovu wa kiakili na kimwili, kula na kunywa vinywaji vinavyoleta usingizi wawapo safarini, kutokuwa na uzoefu wa kuendesha masafa marefu na kutojua barabara vizuri.

"Uzoefu, ulevi na uchovu huchangia kwa kiasi kikubwa ajali za magari binafsi kwa kuzingatia kwamba kwa muda mrefu mtu hajasafiri kwenda kwao, unakuta barabara zimetengenezwa na kuwekewa tahadhari, lakini hajui; mwisho wa siku anatumbukia huko.

"Sababu nyingine ni za kila siku zinazohusu mwendokasi, kupita gari lingine bila kuchukua tahadhari," anafafanua Kamanda Ng'azi.

**JAMII YAONYA**

Elizabeth Stanslaus, mkazi wa Kimara, wilayani Ubungo, mkoani Dar es Salaam, anashauri wanafamilia wanapotaka kusafiri ili kuepuka changamoto mbalimbali ikiwamo ajali, ni vizuri wakasafiri katika vyombo tofauti vya usafiri badala ya kutumia gari moja.

Michael Valentine, mkazi wa Mwenge, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, anasema ndugu wakiamua kutumia gari moja, basi wazingatie kanuni za usalama barabarani na kuchukua dereva mzoefu wa barabara.

"Si kila dereva anaweza kwenda mwendo mrefu, kama umezoea ruti fupi halafu ukaenda safari ndefu huku umebeba familia ni kujihatarisha kwa sababu kuna kuchoka au wakati unaendesha unaanza kukizoea chombo na mwishowe umakini unapungua," anasema.

**AJALI MIAKA 6**

Zikirejewa ripoti za matukio ya ajali za barabarani zinazosababisha vifo vya ndugu kwa wakati mmoja katika kipindi cha miaka sita iliyopita, zinajumuisha:

Juni 24, mwaka huu, wanafamilia wanne waliokuwa wakitokea harusini Dar es Salaam walipata ajali eneo la Bwiko, Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga. Waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo ni Cecilia Luka (mama mzazi wa bwana harusi), Antonio Luka (dada yake), Judith Michael (42) na Godfrey Michael, waliokuwa katika gari dogo aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T 979 CZM. Wote walikuwa wakazi wa Rombo.

Februari 3, mwaka huu, msiba wa aina hiyo ulikumba familia ya ukoo wa Mrema katika Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, baada ya kupoteza watu 16 kwa ajali ya barabarani.

Walikuwa wanasafirisha mwili wa Athanas Mrema (59) kwa gari.

Ajali hiyo ilitokea eneo la Magira Gereza, Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, barabara ya Segera/Bwiko, baada ya lori la mizigo aina ya Mitsubishi Fusso lenye namba za usajili T 673 CUC, kugongana uso kwa uso na basi dogo aina ya Toyota Coaster, lenye namba T 863 DXN (Special Hire) walimokuwa.

Novemba 28, 2023, bibi harusi mtarajiwa Rehema Chao (37) na mama yake mzazi, Agness Chao (75), walifariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria aina ya Toyota Raum, kugongana uso kwa uso la lori la mizigo katika eneo la Kisangara, Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro.

Ajali hiyo ilitokea baada ya Rehema aliyekuwa akiendesha gari hilo, kukwepa shimo na kugongana na lori. Bibi harusi huyo alikuwa akiendesha gari hilo (Raum) kutoka Morogoro kwenda nyumbani kwao Msae-Marangu ili kuwahi harusi yake iliyokuwa ifungwe siku chache zilizokuwa zinafuata jijini Arusha.

Aprili 25, 2023, majira ya asubuhi, watu wanne wakiwamo watatu wa familia moja, walifariki na wengine wawili kulazwa baada ya gari walilokuwa wamepanda kusombwa na mafuriko katika eneo la King'ori, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, wakati wakielekea kwenye mahafali ya binti yao mkoani Kilimanjaro.

Ndugu waliofariki katika tukio hilo ni Martha Metili (40) na mtoto wake Lissa Metili (8) na Collin Lyimo (16).

Watu hao walikuwa wakitumia gari lao aina ya Toyota Noah, lenye namba za usajili 499 DMY, kusombwa katika barabara ya Arusha/Moshi, eneo la Kata Amarura Tarafa ya King'ori, Wilaya ya Arumeru.

Juni 22, 2023, Mrakibu wa Jeshi la Uhamiaji Kurasini, Dar es Salaam, Martin Mhagama (45) na mkewe Rehema Sekhao (40), walipoteza maisha katika ajali ya gari iliyohusisha basi la abiria, mali ya Kampuni ya Kilimanjaro Express na gari dogo aina ya Toyota Corola.

Ajali hiyo ilitokea katika eneo la Majengo, Hedaru, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, wakati ofisa huyo na mkewe wakitokea Dar es Salaam kwenda Moshi.

Julai 4, 2023, walifariki dunia watu wanne wa familia moja wilayani Masasi, mkoani Mtwara, baada ya pikipiki waliyokuwa wakisafiria kugongana na lori aina ya fuso lenye namba za usajili T 522 BBQ.

Agosti 2, mwaka 2023, watu wanne wa familia moja walifariki dunia katika ajali iliyotokea Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Oktoba 11, 2022, Sajini wa Jeshi la Uhamiaji nchini na Ofisa wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Silvester Chambo (36), alifariki dunia kwa ajali ya gari, akiwa na ndugu saba wa familia moja.

Chambo, akiwa anaendesha gari lake aina ya Toyota Corola, lenye namba za usajili T 618 AWP, lililokuwa likitokea Muheza Tanga, liligongana uso kwa uso na Voxywagen lenye namba T 515 DMV, mali ya Honoratus Swai, Mkazi wa Dar es Salaam

INAENDELEA UK.5



Mkazi wa Chole, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, akiteka maji kwenye chemchem hivi karibuni kutokana na eneo lao kutokuwa na huduma ya maji safi na salama. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bil. 31/- yakwamisha miradi 724 ya maendeleo Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

UJENZI wa miradi 724 ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 31 inayotekelezwa mkoani Singida, umekwama kutokana na kuhitaji fedha za ziada.

Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, aliyasema hayo wakati wa kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama cha kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Halima alisema hatapenda kusikia miradi yoyote ya maendeleo inayoibuliwa katika halmashauri za mkoa huo inakwama kwa kisingizio cha kutaka kuongezewa fedha za ziada.

Alisema kuanzia sasa halmashauri zote zinatakiwa kuhakikisha zinakamilisha miradi yake kwanza ikiwamo maboma yote yaliyojengwa kabla ya kuanzisha miradi mipya.

Mkuu wa Mkoa aliagiza madiwani kuwa mstari wa mbele katika kusimamia utekelezaji miradi ya maendeleo badala ya wao kuanza kulalamika kuwa miradi inayotekelezwa katika maeneo yao haikamiliki.

"Madiwani mnatakiwa kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo katika maeneo yenu na miradi hiyo ilete matokeo chanya kulingana na thamani ya fedha," Mkuu wa Mkoa Halima aliagiza.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alielekeza wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kuwa wabunifu katika utekelezaji miradi ya maendeleo ikiwamo kuajiri kwa mkataba wahandisi waliostaafu na mafundi wenye ujuzi wa kujenga, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wake.

Dk. Fatuma alisema anajua kuna uhaba wa watumishi hasa katika kada ya uhandisi, lakini usiwe kisingizio cha miradi kukwama.

Alisema ni muhimu wakurugenzi wakawa na njia mbadala ya kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati na kuzingatia ubora unaotakiwa.

Katibu Tawala alisema miradi yote ya maendeleo ambayo haijakamika lazima iingizwe katika bajeti mpya ili ujenzi wake ukamilike.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega, alishuruku serikali kwa kuipatia fedha nyingi halmashauri hiyo kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maendeleo.

Mkwega alisema tangu aanze kazi ya udiwani hajawahi kuona fedha nyingi zinazotolewa na serikali kama kipindi hiki, hivyo madiwani wana jukumu kubwa la kuhakikisha miradi inakuwa na ubora kulingana na thamani ya fedha.

## Undani ajali zinazoua ndugu wengi pamoja

INATOKA UK. 4

aliyekuwa akitokea Moshi.

Oktoba 11, 2022, watu watano wakiwamo wawili wa familia moja waliokuwa wakienda msibani Kyela, walifariki dunia katika ajali iliyohusisha basi dogo aina ya Coaster na basi la Kampuni ya Kyela Express baada ya kugongana uso kwa uso eneo la Kiwira, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya.

Novemba 26, 2022, Immaculate Byemerwa (49) pamoja na watoto wake wawili, Jolister Byemerwa (17), mhitimu kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Gili ya Kibaha na Janeth Byemerwa (20), mwanafunzi aliyekuwa anasoma mwaka wa tatu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), walipoteza maisha wakitoka katika sherehe ya mahafali Kibaha mkoani Pwani.

Chanzo kikiwa ni gari aina ya Prado Land Cruiser walilokuwa wakisafiria kupoteza mwelekeo na kuacha njia na kuangukia katika bonde. Katika ajali hii kulikuwa na majeruhi mmoja.

Mwezi Aprili, 2018, watu wanane wa familia moja walifariki dunia papo hapo na mmoja kujehuriwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka wilayani Chunya kwenda mjini Mbeya, kugongana uso kwa uso na basi la Kampuni ya Igembesabo katika eneo la Igodima barabara kuu ya Mbeya- Tabora nje kidogo ya Jiji la Mbeya.

Mei 29, 2018, mkoani Rukwa, watu watatu wa familia moja walifariki dunia katika ajali iliyohusisha pikipiki iliyokuwa imebeba wanafamilia hao na basi mali ya Kampuni ya Saratoga.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati anawasilisha bungeni Juni 13 mwaka huu mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25, alisema ajali za barabarani zinagharimu maisha ya watu wengi nchini, akishauri kufanywe mabadiliko ya sheria ili wanaosababisha ajali washtakiwe kwa jinai ya mauaji.

Dk. Mwigulu alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano (2019 hadi Mei 2024), ajali za barabarani nchini zilikuwa 10,093 zikisababisha vifo vya watu 7,639 na kujeruhi watu 12,663, wakiwamo waliopata ulemavu wa kudumu.

"Hebu fikiria, magari binafsi - ajali 3,250, vifo 2,090, majeruhi 3,177. Hebu fikiria, mabasi - ajali 790, vifo 782, majeruhi 2,508. Hebu fikiria, daladala - ajali 820, vifo 777, majeruhi 1,810. Hebu fikiria, taxi - ajali 93, vifo 97, majeruhi 173. Hebu fikiria, magari ya kukodi (sherehe, misiba, na shughuli maalum) - ajali 326, vifo 263, majeruhi 302.

"Idadi hii kubwa ya majeruhi na vifo vya watu kutokana na ajali utadhani nchi iko kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe," alitamka Waziri Mwigulu kwa hisia kali bungeni.

# Waonywa kutanguliza fedha katika utoaji huduma za afya

**Beatrice Shayo,** ARUSHA

MGANGA Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, ameagiza watoaji huduma nchini kuzingatia kuokoa maisha ya wananchi wanapofika katika vituo vya afya badala ya kuweka fedha mbele.

Prof. Tumaini alitoa agizo hilo juzi jioni wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutembelea mahema ya wagonjwa waliokuwa wanapatiwa matibabu katika kambi maalum ya matibabu bure jijini hapa.

"Nitoe rai kwa watumishi wa sekta ya afya tutathmini uhai, hilo ndilo jukumu letu tulilopewa katika dhamana ya kutoa huduma kama muuguzi, mfamasia, daktari. Viapo vinatutaka kutetea uhai, tusiweke mbele fedha," alisisitiza Prof. Tumaini.

Mganga Mkuu wa Serikali alisema watumishi wa kada hiyo wanapaswa kutetea uhai wa wananchi ndipo fedha ifuate na kusisitiza viapo vilivyotolewa kwa watu wote ambao wanatoa huduma katika sekta binafsi na ya umma vinaelekeza hivyo.

Kuhusu kambi hiyo, alisema serikali imeunga mkono jitihada hizo katika kutoa vifaa na dawa na tayari watu zaidi ya 200 wamefanyiwa kipimo cha x-ray na wagonjwa wengine wanaendelea kupatiwa matibabu katika hospitali za serikali.

Alisema hadi juzi waliopelekwa katika hospitali za serikali wamepatiwa msamaha wa matibabu ya zaidi ya Sh. milioni 28 na zaidi ya vipimo 700 kwa siku nne.

Prof. Tumaini alisema kupitia kambi hiyo wamejifunza kwamba wapo waliofika wakihitaji huduma na wengine wakitaka kupatiwa huduma za kibingwa.

"Hospitali zote za halmashauri unapata x-ray na huduma za dharura unazipata huko, tunaendelea kupambana kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi ngazi ya chini ili wasihangaike kwenda umbali mrefu kufuata huduma za afya.

"Wengi waliofika hapa wana changamoto ya kifedha, ukiwa na bima ya afya una uhakika wa kupata matibabu kokote. Bima ya afya ndio suluhu na serikali imejipanga kusaidia wale ambao ni maskini kupata bima ya afya ili kila mwananchi aweze kupata huduma za afya," alisema.

Mganga Mkuu wa Serikali alisema huduma za mkoba zinaendelea na madaktari bingwa wanatoa huduma katika ngazi ya msingi ili kuwezesha wananchi kuzipata.

Alikumbusha jamii kujenga utamaduni wa kuangalia afya zao mara kwa mara kwa kuwa kupitia kambi hiyo, waliobainika kuwa na shinikizo la damu ni wengi, huku wengi wao hawakuwa na taarifa.

Pia alisisitiza jamii kuzingatia mlo kamili wa vyakula na kufanya mazoezi mara kwa mara, ili kujiepusha na maradhi ambayo yanazuilika.

"Ninaomba Watanzania wasipende kutumia dawa ovyo hasa hizi za antibaiotiki mpaka utakapoandikiwa na daktari.

"Ukifanya kinyume utasababisha usugu wa vimelea vya dawa na hatutakuwa na dawa ya kutibia haya magonjwa," alisema Prof. Tumaini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umakini unahitajika katika utekelezaji bajeti 2024/25

**BAJETI** ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24 itafikia ukomo wake kesho, hivyo kuanza mwaka mpya wa fedha 2024/25 ambao serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. Sh. trilioni 49.35

Katika bajeti hiyo ambayo ni ya nne kwa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kunatarajiwa ongezeko la makusanyo na matumizi kwa asilimia 11.2 kulinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24.

Kwa mujibu wa Wizara ya Fedha, ongezeko la bajeti kwa kiasi kikubwa limetokana na kugharamia: Deni la Serikali ambalo limeongezeka kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi, kuongezeka kwa viwango vya riba na kuiva kwa mikopo ya zamani.

Vilevile, ajira mpya; ulipaji wa hati za madai; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; na maandalizi ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027 ikiwamo ujenzi na ukarabati wa viwanja vinatajwa kuchangia ongezeko hilo.

Sura ya bajeti hiyo inaonesha kuwa mapato ya ndani - Serikali Kuu yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 33.254, misaada na mikopo nafuu kutoka washirika wa maendeleo Sh. trilioni 5.131 na mikopo ya kibiashara ndani na nje Sh. trilioni 9.604.

Kati ya Sh. trilioni 49.35 zinazotarajiwa kukusanywa na kutumika, matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuwa trilioni 34.590 na matumizi ya maendeleo Sh. trilioni 14.755.

Ikiwa ni siku moja kabla ya kuanza utekelezaji bajeti hiyo, Nipashe Jumapili tunakumbusha serikali umuhimu wa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika bajeti hiyo.

Hivyo ni pamoja na kukamilisha miradi ya kielelezo na ya kimkakati, kuimarisha rasilimali watu hasa katika sekta za huduma za jamii, kuongeza matumizi ya TEHAMA na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji katika sekta binafsi.

Tunakumbusha pia serikali kuimarisha upatikanaji mbegu bora, pembejeo na zana za kilimo na uvuvi, huduma za ugani na utafiti, uimarishaji malambo na majosho, ujenzi wa maghala na upatikanaji masoko ya mazao na mifugo ndani na nje ya nchi.

Serikali pia imepanga kufungamanisha ukuaji uchumi na maendeleo ya watu kwa kuboresha upatikanaji huduma za afya, elimu na ujuzi na huduma za maji safi na salama kupitia utoaji elimumsingi bila ada, utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati, kuboresha huduma ya maji, kuimarisha elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ununuzi na usambazaji dawa pamoja na ujenzi wa hospitali za wilaya na vituo vya afya.

Nipashe Jumapili tunakumbusha pia uboreshaji mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji kupitia utekelezaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu nishati, usafirishaji pamoja na ununuzi na ukarabati wa ndege, meli na vivuko.

Mbali na vipaumbele hivyo, serikali pia inatarajiwa kupunguza tatizo la ajira nchini kwa kutoa ajira mpya kwa wananchi, hususan vijana waliohitimu vyuo vikuu na maeneo mengine ya kitaaluma.

Vilevile, tunakumbusha ahadi iliyotolewa ya kulipa madeni ya wazabuni, watumishi na mifuko ya hifadhi ya jamii ambako Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebainisha kuwapo kwa deni kubwa na la muda mrefu.


Nipashe Jumapili tunaamini kuwa, bila kuwapo nidhamu katika matumizi, utekelezaji bajeti hiyo ya serikali hautafanikiwa, hivyo kuna haja serikali kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha utawala bora katika usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Ndiyo maana tunasisitiza mamlaka husika za serikali kuongeza umakini katika kuyatekeleza mambo haya muhimu yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/25.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



# Tusome kanuni za INEC, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura

Na Sabato Kasika

**TUME** Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) inatarajia kuanza uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura Julai 20 mwaka huu, ikianzia mkoani Kigoma kisha kuelekea mikoa mingine.

Awali kazi hiyo ilipangwa kuanza Julai Mosi, lakini baadaye tume ikaahirisha. Itaanza mwishoni mwa Julai, muda ambao ninadhani si vibaya wananchi kuendelea kufuatilia na kujifunza kanuni hizo.

Katika uboreshaji huo, tume imejipanga kutumia siku saba kwa kila mkoa, huku wapigakura wakiboresha taarifa zao na wengine kuandikishwa kwa ya kwanza kuwa wapigakura.

Wakati INEC inajiandaa kwa ajili ya kazi hiyo, ninadhani ni vyema kukumbusha Watanzania baadhi ya yale yaliyomo katika Kanuni za Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura za Mwaka 2024.

Kwa kawaida katika mkusanyiko wa watu, huwa kuna mambo mengi yanayoweza kutokea yakiwamo hata ya kuvuruga shughuli na kusababisha usumbufu kwa wengine.

Hapa ninalenga kugusia Ibara ya 56 ya kanuni hizo ambayo inaeleza, "Mtu yeyote anayekataa kuondoka katika eneo lolote linalotumiwa kwa ajili ya shughuli za uandikishaji wapigakura au masuala yaliyoanishwa katika kanuni hizo, baada ya mtendaji wa uandikishaji kumtaka kuondoka katika eneo hilo, anatenda kosa."

Ibara ya 57(a) inasema, "mtu yeyote ambaye bila kuwa na mamlaka halali, anaharibu zana za uandikishaji zilizobandikwa; au (b) anachapa au kusambaza zana yoyote ya uandikishaji bila idhini ya tume au ofisa mwandikishaji, anatenda kosa."

Ibara ya 58 inasema, "Mtu yeyote ambaye anatenda kosa chini ya kanuni hizo, akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 300,000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja."

Kanuni hizo zinaelezea mengi ambayo jamii inapaswa kuyazingatia wakati wa zoezi hilo litakapoanza. Hivyo, nimejaribu kutaja machache, lakini jambo la msingi ni kila mmoja kuzisoma.

Ni muhimu kila mmoja kuzisoma na kuzizingatia, ili kuepuka kuingia katika makosa na kupigwa faini au kufungwa kwa mambo ambayo wakati mwingine kama yakizingatiwa, mtu inaweza kuwa salama.

Kwa mujibu wa tume, mawakala wa vyama vya siasa wanaruhusiwa kuwapo kwenye vituo vya kuandikisha, hao ndio ambao baadhi yao wakati mwingine hujikuta wakifanya vurugu au jambo ambalo ni kinyume cha utaratibu.

Hivyo, ni vyema wakasoma kanuni hizo na kuzielewa na kuzifanyia kazi ili wawe sehemu ya kufanikisha kazi ya uboreshaji daftari hilo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Tume inasema imejipanga kuandikisha wapigakura wapya 5,586,433 nchi nzima na kuboresha taarifa za wapigakura 4,369,531. Lakini ninadhani lengo hilo haliwezi kufikiwa iwapo jamii haitazingatia kanuni.

Wapo baadhi ya vijana ambao hutumiwa na baadhi ya wanasiasa kuanzisha vurugu katika kampeni au kushushiana bendera kwa manufaa binafsi.

Hayo na mengine mengi, ni muhimu kuyaepuka wakati wa uboreshaji daftari hilo ili kutoingia katika matatizo.

Ikumbukwe kuwa wakati wa uboreshaji daftari hilo, kuna makundi ambayo yatapewa kipaumbele katika foleni, yakijumuisha watu wenye ulemavu, wajawazito, wagonjwa, wazee na kinamama wenye watoto wachanga, hivyo haitakuwa sawa mtu mzima kukataa kuwapisha.

HABARI KITAIFA

## Raia Iran wapiga kura Dar Uchaguzi wa Rais

**Na Mwandishi Wetu**

RAIA wa Iran wanaoishi nchini wamepiga kura za uchaguzi wa Rais mpya wa nchi hiyo kupitia Ubalozi wa Iran, jijini Dar es Salaam.

Uchaguzi huo wa muhula wa 14 wa urais wa Iran ulifanyika juzi kwa ajili ya kumpata mrithi wa Ebrahim Raisi aliyefariki dunia kutokana na ajali ya ndege hivi karibuni.

Uchaguzi huo ulifanyika kwa wakati mmoja na Iran katika nchi mbalimbali na kwa Tanzania, Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran jijini Dar es Salaam uliandaa uchaguzi kwa Wairani wanaoishi Tanzania kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

Balozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran Tanzania, Hossein Alvandi, akiwashukuru Wairani wanaoishi Tanzania waliofika ubalozini kushiriki katika uchaguzi wa Rais, alisema kupiga kura kwa Wairani ni wajibu wa kitaifa na hisia ya kujitolea kwa nchi yao na kushiriki katika maendeleo ya taifa.

Rais Raisi alifariki dunia Mei 19 mwaka huu kutokana na ajali ya helikopta iliyokuwa ikimbeba.

Kwa mujibu wa Katiba ya Iran, katika tukio la kifo cha Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais anachukua madaraka na majukumu kwa muda mfupi na anatakiwa kuhakikisha ndani ya muda usiozidi siku 50, Uchaguzi wa Rais mpya unafanyika.

Katika uchaguzi huo wa Iran, Makamu wa Kwanza wa Rais hajagombea na uchaguzi ulihusisha wagombea wanne kutoka vyama mbalimbali vya kisiasa.

Katika uchaguzi huo, wagombea hao wanne ni Mohammad Bagher Ghalibaf, Saeed Jalili, Mwanamageuzi Masoud Pezeshkian na mwenye msimamo wa kati Mostafa Poormohammadi.

Mgombea anahitaji kupata zaidi ya asilimia 50 ya kura ili kushinda hatua ya kwanza, duru ya pili kati ya wagombea wawili wa juu itafanyika wiki ijayo.



Mwendesha Pikipiki akiwa amepakia viroba vya Mkaa akitafuta wateja katika Kijiji cha Masaki Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## NHIF, ZHSF zaingia makubaliano utoaji huduma kwa wanachama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) zimetia saini mkataba wa makubaliano ya utoaji huduma za matibabu kwa wanachana wao.

Mkataba huo unalenga kutoa huduma kwa wanachama wa ZHSF kupitia vituo vilivyosajiliwa na NHIF Tanzania Bara kuanzia Julai Mosi mwaka huu.

Hatua hiyo ni utekelezaji uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma za matibabu wanapozihitaji bila kikwazo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema juzi jijini hapa kuwa hatua hiyo ni katika kuhakikisha ZHSF inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Na. 1/2023.

"Na kwa kutambua uzoefu wa NHIF, katika uendeshaji mfumo wa bima ya afya nchini, Julai Mosi 2024, ZHSF itaanza rasmi majukumu yake kwa kuhudumia wanachama na wategemezi wake kupitia vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na NHIF Tanzania Bara," alisema Konga.

Alisema ili kufanikisha huduma kwa wanachama hao, NHIF na ZHSF zimetia saini mkataba wa makubaliano wa ushirikiano katika utoaji huduma kwa wanachama wake.

"Hatua hii inatokana na uzoefu, wigo mpana wa vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na NHIF nchi nzima," alisisitiza Konga.

Alisema NHIF imekamilisha hatua mbalimbali za maandalizi na utayari wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa ushirikiano ili kuhakikisha wanachama hao wanapata huduma bila changamoto yoyote.

Mkurugenzi huyo alisema hatua ilizokamilisha NHIF ni pamoja na kutoa taarifa kwa watoa huduma wote kuhusu suala hilo na kuwa tayari kuhudumia wanachama. Alisema ofisi zote za NHIF zilizoko katika mikoa ziko tayari na zimejipanga kutoa huduma na kutoa msaada utakapohitajika. "Mifumo ya utambuzi imeimarishwa zaidi ili kurahisisha utambuzi wa wanachama wanapofika katika vituo vya kutolea huduma, kufanya malipo kwa watoa huduma kwa wakati pindi wanachama watakapopata huduma za matibabu katika vituo husika, kuandaa ofisi kwa ajili watumishi wa ZHSF watakaokuwa wanahudumia wanachama kwa upande wa Tanzania Bara," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ZHSF, Yaasin Juma, alisema kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria Namba.1 ya 2023, mfuko umepewa uwezo wa kuwafikishia wanachama wake huduma za afya nje ya Zanzibar.

Alisema kwa kuanzia ZHSF imeanza kuwafikia wanachama wake walioko Tanzania Bara.

"Tukio la leo linaakisi utekelezaji wa masharti ya sheria hiyo. Hivyo basi, mafanikio haya ya kufikia makubaliano na wenzetu wa NHIF ni ya kujivunia, kwani yatawawezesha wanachama wetu kupata huduma za afya wakiwa Tanzania Bara kwa kutumia kadi za ZHSF," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wanategemea mashirika yao kama ZIC na PBZ ambayo yanafanya kazi Tanzania Bara na wategemezi ambao wachangiaji wao wako Zanzibar watafaidika na huduma hizo.

## DC atangaza vita uharibifu miradi ya maji

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka amesema hatosita kumchukulia hatua kali za kisheria mtu yeyote atakayebainika kuharibu miradi waliyokabidhiwa na Shirika la World Vision.

Miradi hiyo iliyokabidhiwa jana na shirika hilo inajumuisha Mradi wa Maji katika Kijiji cha Zombo uliogharimu Sh. milioni 102, Mradi wa Maji Kijiji cha Madudumizi Sh. milioni 100.5, Mradi wa Maji Kijiji cha Ulaya Mbuyuni Sh. milioni 145.7 na jengo la zahanati lililogharimu Sh. milioni 183.

Akizungumza katika uzinduzi uliofanyika wilayani Kilosa juzi, Shaka alisema jukumu lililobaki ni la wananchi kuitunza miundombinu hiyo kwa wivu mkubwa ili vizazi vijavyo vifaidi matunda yake.

"Tukiitunza itadumu, tusipoitunza itaharibika na kesho tutaonekana hatuna fadhila, nina matumaini sisi tutakuwa sehemu ya kuilinda.

"Kipekee nishukuru Shirika la World Vision kwa kutufikia Kilosa, hii inatokana pia na sera nzuri za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuita kila siku wadau kushiriki katika shughuli za maendeleo," alisema.

Mratibu wa Word Vision, Elisei Chilala, alishukuru uongozi wa wilaya hiyo kwa ushirikiano na mwitikio mkubwa tangu walipoanza kutekeleza miradi hiyo mpaka kukamilika kwake. Alifafanua kuwa miradi hiyo imetekelezwa na shirika hilo nchini kupitia Mradi wa Maendeleo Ulaya ambao umejikita katika masuala ya elimu, maji, lishe na utetezi katika masuala ya ulinzi na usalama wa mtoto.

Chilala alisema katika Kijiji cha Zombo, Mradi wa Maendeleo wa Ulaya ulihusika katika kuchimba kisima, ujenzi wa tangi la maji, kibanda cha pampu, kuweka umeme wa jua na kusambaza maji kijijini na shuleni na kuweka vituo 10 vya kuchotea maji.

"Katika Kijiji cha Madudumizi, Mradi wa Maendeleo Ulaya ulichimba kisima kirefu, kujenga kibanda cha pampu, kuweka umeme jua, kusimika matangi mawili ya maji na kusambaza maji kijijini, shuleni na zahanati na una jumla ya vituo saba vya kuchotea maji.

"Katika Kijiji cha Ulaya Mbuyuni, Mradi wa Maendeleo wa Ulaya ulikarabati kisima kilichokuwapo, ujenzi wa tangi la lita 50,000, kuweka umeme jua, kukarabati kibanda cha pampu, kusambaza maji na kuyapeleka Shule ya Sekondari Ukwiva na Shule ya Msingi Ulaya Mbuyuni, na una jumla ya vituo vitano vya kuchotea maji," alisema.

Alisema katika mradi wa zahanati pia walijenga jengo la mama na mtoto lililogharimu Sh. milioni 87 na kuchangia ununuzi wa vifaa tiba vya Sh. milioni saba ambavyo ni vitanda vya kujifungulia viwili, vitanda vya hospitalini viwili, vitanda viwili vya wagonjwa viwili, mashine moja ya kidigitali ya BP, mizani miwili ya watoto na vifaa vya kujifungulia seti mbili.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo, akiwamo Hadija Iddi, walisema miradi hiyo imeongeza urahisi katika upatikanaji huduma za maji, afya na elimu.

Hadija alisema kuwa kabla ya huduma hizo walilazimika kuvuka maji kufuata huduma za afya na kuchangia baadhi ya wagonjwa kufariki dunia njiani.

Idd Kyande alishukuru shirika hilo kwa kuwapelekea huduma hizo ikiwamo ya maji katika baadhi ya shule, akisifu inasaidia wanafunzi kupata maji safi na salama.




Wateja wakichagua vyombo vya nyumbani kwa wafanyabiashara wa vyombo Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

UCHAGUZI 2024, 2025

# TAKUKURU yasuka mkakati kunasa watoaji, wapokeaji rushwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kamishna Salum Hamduni, amesema kuwa katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, wamejizatiti kikamilifu kuzuia na kupamba na vitendo vyote vya rushwa.

Kamishna Hamduni alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi wakati akifungua warsha ya wahariri wa vyombo vya habari kujadili namna ya kudhibiti vitendo vya rushwa katika uchaguzi huo.

Alisema kuwa ili kukabiliana na vitendo vya rushwa katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani TAKUKURU inao wajibu wa kuja na mkakati wa kukomesha vitendo hivyo.

"Pamoja na jitihada za serikali, TAKUKURU nayo haijabaki nyuma ambapo kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329, imejizatiti kikamilifu kuendelea kutimiza wajibu wake wa kuzuia na kupambana na rushwa nchini, ikiwamo katika uchaguzi," alisema

Kamishna Hamduni alisema kuwa baadhi ya mambo ambayo taasisi hiyo inapaswa kufanya ni pamoja na kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi ili wachague viongozi waadilifu.

Pia alisema TAKUKURU itashirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha wananchi kutojihusisha na vitendo vya rushwa ikiwamo rushwa katika uchaguzi.

"Warsha hii ni sehemu ya utekelezaji huu na bado tutakutana na makundi mengine ya wadau ili kujipanga kwa pamoja," alisema.

Alisema jambo lingine wanalopaswa kufanya ni kufanya utafiti na udhibiti kwa lengo la kubainisha mianya ya rushwa katika uchaguzi na kushauri namna bora ya kuiziba.

Kamishna Hamduni alisema taasisi itachukua hatua za haraka kuzuia vitendo vya rushwa na kuchukua hatua za kisheria kuchunguza na kuendesha mashtaka kwa watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Vilevile, alisema vyombo vya habari vinao wajibu wa kufahamisha wananchi athari za rushwa katika uchaguzi.

Alitaja athari hizo ni pamoja na kupatikana viongozi wasio waadilifu wanaojihusha na vitendo vya rushwa pamoja na kutozingatia misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo.

"Vilevile, rushwa inadhoofisha utawala bora na demokrasia, ambapo baadhi ya wananchi mwenye sifa za uongozi bora hushindwa kugombea au kutoteuliwa kwa kutokuwa tayari kutoa hongo," alisema

Alitaja athari nyingine ni kusababisha uvunjivu wa amani kutokana na migogoro ya mara kwa mara ya kisiasa na kusababisha taifa kuendelea kugubikwa na rushwa.

"Kusababisha wananchi kukosa imani na serikali na hata kusababisha machafuko na la kusikitisha zaidi ni kuwa na hongo ya fedha, nguo, chakula anayopewa mtu ili apige kura, inadhalilisha utu," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Takukuru Kamishina, Salum Hamduni

Alisema TAKUKURU inaamini madhara hayo yanaweza kuepukika pale tu washiriki wa warsha hiyo watakapoamua kujadili na kuandaa mkakati wa kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi.

"Ushiriki wenu wahariri wa vyombo vya habari katika warsha hii ni ishara ya wazi ya kuunga mkono jitihada za serikali kudhibiti vitendo vya rushwa nchini hususan kwenye uchaguzi wetu," alisema Kamishna Hamduni.

**UCHAGUZI 2020**

Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa TAKUKURU, Sabrina Seja, akiwasilisha mada kuhusu udhibiti wa rushwa, alisema kuwa uchambuzi wao kuhusu viashiria vya rushwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 umebaini kuwa rushwa ya vyakula, vinywaji na pombe ilikuwa kwa asilimia 13.3, fedha (asilimia 64.4), mbolea asilimia 2.2 na vitu au vifaa (asilimia 20).

Alisema rushwa inagusa mchakato mzima wa uchaguzi kuanzia uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, kujumlisha na kutangaza matokeo hadi ushughulikiaji malalamiko baada ya uchaguzi.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma TAKUKURU, Joseph Mwaiswelo alitaka jamii ipinge vikali vitendo vya rushwa wakati wote kwa kuwa vikiachwa, ni hatari kwa maendeleo ya taifa.

Alisema kuwa kwake fasili sahihi ya neno 'uchaguzi' ni kuamua kuwa masikini au kupata maendeleo kupitia viongozi ambao wananchi wanaamua wawape kura zao.

# Majaliwa apongeza uongozi mpya TEC



**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametoa pongezi kwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kupata safu mpya ya uongozi.

Baraza hilo limepata Rais, Makamu wa Rais na Katibu kwenye uchaguzi uliofanyika tarehe Juni 21 mwaka huu.

Majaliwa amesema serikali inaahidi viongozi hao kuwa itaendelea kutoa ushirikiano kwa baraza hilo ili watekeleze majukumu yao ya kiroho na kijamii kikamilifu kwa ustawi wa Kanisa Katoliki na taifa kwa ujumla.

Viongozi waliochaguliwa katika uchaguzi huo ni Mhashamu Wolfgang Pisa, Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi (Rais), Mhashamu Eusebius Nzigilwa, Askofu wa Jimbo Katoliki la Mpanda (Makamu wa Rais) na Padri Charles Kitima, Padri wa Jimbo Katoliki la Singida (Katibu Mkuu).

Waziri Mkuu alisema jana kuwa kukamilika kwa safu hiyo ya uongozi ndani ya Kanisa Katoliki ni ishara kwamba kanisa linaendelea kujipambanua kuhusu umuhimu wa ngazi za uamuzi zinazosaidia uratibu na usimamizi wa kanisa.

"Mungu awabariki viongozi wote na kuwasimamia katika majukumu yenu," alisema Waziri Mkuu kupitia taarifa iliyotolewa na ofisi yake jana.

MAISHA
JUNI 30, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili






Ukurasa 15



# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| W | | N | D | E | G | E |
| A | | | | L | | N |
| T | | B | E | E | | D |
| A | N | A | | Z | E | E |
| L | | N | O | A | | L |
| I | | D | | | | E |
| I | M | A | R | A | | A |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


MEI, ILI, NTA, LOA, ELEZA, AKILI, SIASA, IAMKE, SHANGWE, ACHANGE

## AMSHA AKILI


HAYA, LEO TUPO NA MCHEZO WA NAMBA, HEBU TUONE UNAVYOJUA KUHESABU: KILA NAMBA INA VIBOKSI VIWILI (KABLA NA BAADA YA NAMBA), UNACHOTAKIWA KUFANYA NI KUJAZA NAMBA INAYOANZA KABLA YA NAMBA ILIYOPO NA NAMBA BAADA YA ILIYOPO. MFANO: 24 **25** 26

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 25 | | | 11 | |
| | 72 | | | 52 | |
| | 43 | | | 32 | |
| | 16 | | | 20 | |
| | 90 | | | 67 | |
| | 58 | | | 88 | |


## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## CHEKA



### Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanagu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho umke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mke akitoa siri za ndani jitafakari!

MPENZI Msomaji, bado tunaendelea kujadili vituko ndani ya ndoa zetu. Ukiona mwanandoa anatoa siri za ndani, hilo ni tatizo kubwa.

Jamaa mmoja akatuma ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani akisema: Mimi naitwa Jumanne (jina la pili tunalo), ninapatikana Mlandizi, Pwani.

"Nimeoa mke ila cha ajabu mambo yetu ya ndani huwa anayapeleka kwao, inafikia kipindi mengine yanaleta chuki kwa ndugu zake. Nikimwonya ataomba msamaha. Lakini siku inayofuata atarudia tena, mpaka sasa kumekuwa na chuki kubwa dhidi yangu mpaka ninakosa amani na ndoa yangu. Ninaomba ushauri)".

Msomaji wangu, nimejaribu kupata maoni toka kwa baadhi ya watu kumshauri jamaa huyu.

Naitwa Alphonce John. Baba huyu ambaye mkewe anaweka mambo ya kifamilia sebuleni (hadharani), afanye yafuatayo ili kutibu hali ya mkewe;

Yeye mwenyewe baba ajichunguze kasoro zake kiutawala na kiuchumi zinazopelekea mke kutoa siri zao nje.

Huyu baba ampende mkewe kwa pendo la dhati. Upendo hauhitaji fedha, ni jambo la hulka tu.

Mipango ya kifamilia aipange mwenyewe asimshirikishe mkewe kwa kipindi cha miezi kadhaa, aongeze utendaji kazi. Mke aone tu anaambiwa kutenda bila kushirikishwa ndio atapata funzo la kuacha kuanika yale ya familia.

Huo ndio ushauri wa msomaji wetu aliompa ndugu yetu huyo kuhusiana na sekeseke hilo. Binafsi nilimshauri mengi ila hapa nikumbushie machache. Kwanza, nilitoa tafsiri ya tabia kama ilivyotoholewa katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu, toleo la pili la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Tabia: Ni mazoea yanayotokana na kurudiarudia hali, mwenendo au matendo.

Kwa tafsiri hii, ninajaribu kuona ukweli unaojitokeza katika malalamiko ya jamaa hapo juu kwamba tabia ya mkewe ya kutoa habari za ndani ya familia kwa watu wengine imekuwa inajirudiarudia hata pale anapomkanya mara kwa mara.

Baada ya kupata ujumbe wa kijana huyo kupitia simu ya kiganjani, nilimpa ushauri ufuatao; kwamba hiyo ni tabia aliyotoka nayo huko kwao.

Ndio maana kabla ya kuoa yafaa uchunguze tabia ya mwenzio. Ingawa tabia zingine hujificha au ni vigumu kuzirekebisha kutokana na kujikita kwenye uasili, lakini jitahidi, pambana na ikiwezekana itisha vikao vya ndugu aonywe, anaweza kubadilika.

Ni ushauri niliompa kwa haraka haraka, lakini bado nilidhani tatizo la bibie huyo lina chimbuko, si bure. Kijana huyu akijaribu kuchimbua uasili wa familia ya mkewe, anaweza kugundua kwamba huenda tabia hiyo ya kuvujisha siri za ndani ya nyumba, amerithi toka kwa mama yake mzazi, au imeanzia kwa bibi mzaa baba au mzaa mama au upande wa baba na kadhalika.

Huo ni mnyororo ambao hauwezi kukatika labda kwa maombi.

Na tabia, kwa maandiko ya Mungu ni roho. Ni kitu kinachotoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine na kuleta madhara.

Kwa mfano, kama mama mzazi wa binti alikuwa na tabia hiyo, na binti wakati anakua alikuwa akiona mama yake akifanya vituko kama hivyo, kwanini binti asiiige?

Chanzo cha matatizo wakati mwingine ni wazazi wetu. Kama wazazi hawakuwalea vyema watoto, matokeo yake ndio hayo, huwa mwendelezo wa madhara hata ukubwani.

Jamaa anasema humkanya mkewe, anaona kabisa amemwelewa lakini baada ya muda hurudia makosa yale yale. Hata yeye mwenyewe (binti) anajishangaa kwanini anarudia aliyokatazwa. Hiyo ni roho inayomfuatilia msichana huyo ambayo inatokana na misingi mibovu aliyokulia.

Hata Mungu ameweka wazi katika moja ya maandiko yake kuhusu misingi kwamba kama haikuwekwa imara, lazima italeta madhara na huwezi kumlaumu mtoto ambaye hukumjenga kitabia.

Anasema; "Misingi ikiharibika, mwenye haki atafanya nini? (Zaburi 11: 3). Mtoto anayo haki ya kuishi maisha mazuri yenye tija. Mzazi ndiye mwenye wajibu wa kumjengea misingi mizuri pamoja na serikali kwa maana ya malezi bora. Sasa kama mtoto hakuandaliwa misingi mizuri ya malezi, akiharibika kitabia, nani wa kulaumiwa?

Msomaji wangu, kabla ya kuoa au kuolewa kwenye familia fulani, chunguza kwanza. Mfano, tabia; je, ni familia ya aina gani? Wacha Mungu, walevi, waabudu matambiko, washirikina, wambeya, wahuni, waasherati, wafitini, wana wivu, wapole na kadhalika.

**Je, una jambo la kimaisha linakutatiza? Tuma ujumbe mfupi 0715268581, pia ipo WhatsApp Au Email: fwingia@gmail.com**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Hasidi ana hila lakini anacheka na wewe

USINIPUNGUZIE mwendo kwa sababu heshima na tamaa havikai nyumba moja.

Ngoja nikuambie ukweli. Ukitaka kufikia mafanikio yako katika maisha na hata masuala ya uongozi, chagua moja.

Sijui unanielewa au niongeze sauti! Ni hivi; usihusudu wala kuingiwa na tamaa na nyakati za watu.

Sikiliza ndugu yangu, jenga tabia ya kuheshimu nyakati za watu kwa sababu nyakati huzunguka. Pale mahali hazina yako ilipo, ndipo moyo wako ulipo.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya haya ninayoyasema na uhusiano wako na Mungu. Sasa sijui umeyaweka wapi?

Kama ndivyo, basi ni muhimu tuheshimu nyakati za watu, ili na wewe ujenge nafasi ya kuheshimiwa wakati wa nyakati zako.

Wako wanaodiriki kusema "kama maisha ninayo, watoto ninao na mali ninazo, hivi ninahitaji nini kingine?" Wanasahau kuna nyakati, wanasahau kuna Mungu aliyewatoa sehemu moja kwenda nyingine.

Hawakumbuki ni yeye aliyewavusha. Acha kiburi ndugu kaka, acha kiburi dada! Ni wangapi waliotafuta mali na kujilimbikizia utajiri wa kufuru; leo wameshushwa cheo, walikutana kile kinachoitwa uteuzi na utenguzi?

Ubaya huwa haujifichi. Yaani huna tofauti na wale ndugu wanagombania, wanatesa watoto au familia ya mwenziwe.

Unadiriki kusema hadharani tena kwa majigambo, haiishi mpaka iishe. Unakimbilia kupeleka kesi mahakamani ili nini? Vitu vya ulimwengu huu visikugombanishe.

Mara umenunua kiwanja unachapisha mtandaoni, unaanza kujenga unaweka maendeleo ya ujenzi mtandaoni. Mwisho wa siku ujenzi unakwama!

Ndugu yangu, wakati mwingine hufanikiwi kwa sababu unatangaza ndoto zako kabla hazijawa! Usisahau siyo kila mtu anafurahia mafanikio yako.

Labda hujanielewa. Hizo ndoto zako za kutaka ukubwa, cheo na umaarufu hakuna tatizo. Ni mfululizo wa picha, mawazo, mihemko na hisia ambazo hutokea akilini kwa kawaida bila makusudi.

Mambo yote hayo huja katika hatua fulani za usingizi; na wakati mwingine zikawa ni ndoto za mchana kweupe.

Usitangaze ndoto yako, tangaza matokeo, vinginevyo utaishia kuuzwa utumwani kama Yusufu. Aliota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia.

Historia isikuzuie kutimiza ndoto yako. Ni muhimu kuwa na utamaduni wa kuheshimu ndoto zetu, hata kama tunadhani kuwa ni ndogo kama vile ndoto ya kumiliki aina fulani ya mali.

Wengi husema wanataka kutimiza ndoto zao, hata hivyo ni wachache hufanikiwa kutimiza ndoto zao.

Kwa kuwa binadamu tuna ndoto tofauti. Ni ngumu kuwa na kanuni moja ya jinsi ya kufikia ndoto zetu, hata hivyo uzoefu unaonesha mambo kadhaa ambayo watu wengi waliofikia ndoto zao wamefanya.

Kuota ndoto ya mabadiliko ya maisha yako, si tu kuwaza au kutamani kufikia hali fulani, bali kuota kwa usahihi ni kutengeneza picha kichwani ya hali unayotaka kufikia au mambo unayotaka kuyapata.

Mungu hawezi kukuacha ukafa bila kutimiza ndoto zako, utaona unapita kwenye misukosuko mingi lakini bado unaishi.

**"Wako wanaodiriki kusema "kama maisha ninayo, watoto ninao na mali ninazo, hivi ninahitaji nini kingine?" Wanasahau kuna nyakati, wanasahau kuna Mungu aliyewatoa sehemu moja kwenda nyingine.**

Wakati mwingine Mungu hutuma malaika waje wakusaidie bila wewe kujua. Ni kama ule wakati wa Ibrahimu, alikuwa katika shida na mkewe Sarah, hawakupata mtoto, malaika wakaja kwake wakamwambia Sarah atapata mtoto, ni kama kipindi cha Sodoma na Gomora, malaika wakaja wakamwokoa Rutu na familia yake.

Wabaya wako ndio watakuwa viongozi wa kupiga kofi kwenye mafanikio yako. Halafu iko siku moja wabaya wako watafitinishana katika hila zao.

Cha ajabu ni kwamba inaweza ikatokea wewe ndio ukawa msuluhishi wao. Ninasema hivi, wachekee wabaya wako ili wasijue kama unajua ubaya wanaokufanyia.

Wengine waache walalamike. Hawalalamiki ili wasaidiwe namna ya kuishi. Wanalalamika angalau wasinyang'anywe haki yao.

***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com
Simu: +255 715 545 490**

# HARUSI



Shangwe na nderemo vilisikika katika ukumbi wa Edema uliopo mjini Morogoro, katika sherehe ya kumuaga na kumtakia kheri kwa maisha mapya ya ndoa, Happy Bisoma. Sherehe ilifanyika Juni 22, mwaka huu na ndoa takatifaku ilifungwa Juni 30.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo




## VAA SIMPO

MAVAZI ni moja ya pambo linalomfanya mtu kuwa na muonekano tofauti na kumpatia utu wake.

Mara nyingi uchaguzi wa mavazi yanamfanya mtu husika kupendeza au la, kama akichagua mavazi sahihi yanayoendana na muda.

Hata hivyo, wanaume wana tatizo la kutochagua mavazi, badala yake wanavaa ili kujilinda na macho ya watu pekee.

Kutokana na hali hiyo wanajikuta wakivaa nguo ambazo hazilingani kuanzia umbo,rangi na hata mtindo .

Leo tutaangalia namna ya kuvaa nguo za kawaida, lakini ikakutoa vizuri.

**CHAGUA RANGI YA NGUO**

Kama una nguo za kawaida ndani unaweza kutokaukiwa umependeza ukiwa umechanganya rangi.

Nguo za rangi nyeusi zinafaa kuwa nazo kwani ni nzuri ukichanganya na rangi ikiwa suruali, shati au fulana.

Mwanaume anapovaa suruali nyeusi inamtoa bomba hasa akichanganya na rangi nyingine za nguo.

Mfano anapovaa Suruali nyeusi, shati ya rangi yoyote inamfaa na kumng'arisha zaidi.

Akivaa shati au fulana nyeusi, hatokuwa na kazi ya ziada kutafuta suruali kwani akivaa jeans, au suruali ya kitambaa ya rangi yoyote lazima itamtoa bomba.

Kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa, hakikisha nguo zako zinaendana na vipindi vya majira ya mwaka, hapa unatakiwa kuwa makini na jambo hilo ili kuepusha na usumbufu.

Wakati wa kipindi cha joto, unatakiwa kuvaa nguo zinazoruhusu mwili kupumua na wakati wa baridi vaa zenye uwezo wa kuhifadhi joto.

UREMBO
Na Mary Geofrey

# Unasafishaje kucha?

KUCHA ni kiungo muhimu kwenye mwili wa binadamu kwa sababu huwa ni utambulisho wa siri kwa mtu husika.

Muonekano wa kucha zako ndio utambulisho wa jinsia yako kama ni mwanaume au mwanamke wa aina gani hasa suala la usafi.

Kutokana na umuhimu huo ni vizuri kujali afya ya kucha zako ili kuhakikisha zinakuwa katika matunzo mazuri.

**Jinsi ya kusafisha**

Wekeza vifaa vya kisasa vya kutunzia kucha.

Tumia brashi ya kucha kwa kusugua chini ya kucha na kuutoa uchafu na kufikia sehemu ngumu ambapo uchafu unajirundika.

**Unaweza tumia mswaki ukiwa hauna vifaa vya kisasa.**

Tumia maji moto na sabuni kwa kunawa mikono.

Anza kwa kusugua chini kabisa kwa kushikilia brashi chini na sugua kuanzia nyuma kuja mbele pole pole, kisha juu ya kucha fanya hivyo kwa kuzunguka.

Toa rangi kwa kuloweka pamba kwenye 'polish remover' na usugue kwa vidole vyenye hinna huna haja ya kuitoa.

kwa vidole vya afya na nguvu vipumzishe kwa kutumia polish kila baada ya wiki kadhaa mara baada ya kuondoa rangi yako.

Loweka kucha na maji kwenye bakuli au sinki ikiwa na maji ya uvuguvugu na pitisha sabuni ya kunawia mikono.

Suuza kwa maji ya uvuguvugu au yalikua kwenye chombo yaani jimwagie, kisha zifute na taulo laini.

Kisha tumia kifaa cha kukatia kucha maana muda huo zitakua laini au kifaa cha kuzipunguza kuweka sawa kama hauzikati.









MAPISHI
Na Mary Geofrey

# Pika kuku laini

KUKU ana mapishi ya aina mbalimbali ya kumpika na ukafurahia mlo wako.

Katika safu ya leo nitafundisha namna ya kupika kuku laini na mwenye ladha nzuri.

Kuku laini unaweza kula chakula cha asubuhi, mchana au jioni.

**Mahitaji**

Kuku nusu kilo moja, asali vijiko vinne, sukari kijiko kimoja na soya sauce nusu kikombe.

Mahitaji mengine ni tangawizi vijiko viwili vya chai, kitunguu saumu vijiko viwili vya chai, chili sauce vijiko vitatu vya mezani, chumvi kiasi na pilipili nyekundu kiasi.

Kadhalika utahitaji mafuta ya olive vijiko vitano vya chakula Currypowder kijiko kimoja cha chai, coriander powder kijiko kimoja cha chai na ndimu moja.

**Namna ya kutengeneza**

Changanya pamoja sukari, asali, soya sauce, tangawizi, kitunguu saumu na chili sauce kwenye kibakuli kidogo.

Safisha kuku, mkaushe maji, mkate vipande vidogo vidogo muweke kwenye kikaangio, mnyunyizie chumvi, pilipili hoho nyekundu na ndimu kiasi.

Weka mafuta jikoni kisha weka kuku na anza kumgeuza geuza kuku mpaka mafuta yapate moto, usiache kugeuza mpaka kuku awe wa kahawia.

Weka viungo vilivyobaki currypowder na coriander powder, koroga kwa dakika 5.

Mwisho mwagia sosi uliyoandaa, usifunike. Pika hadi iwe nzito.

Epua nyama ya kuku na jirambe na familia.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# NI HATARI KUJENGA NYUMBA KWENYE UDONGO WA MFINYANZI

KUNA mambo mengi ambayo huchangia kuleta athari kwenye nyumba na hili tumekuwa tukijifunza kutokana na maelezo ya watalaamu mbalimbali wa sekta hii.

Watalaamu hao wamekuwa wakisema kwamba kama ilivyo kwa vitu vingine kukumbana na changamoto mbalimbali, uchaguzi wa eneo la ujenzi wa nyumba pia unahitaji umakini mkubwa.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimekuwa vikisisitizwa na wataalamu hao ni uzingatiaji katika ununuzi wa kiwanja na kujenga nyumba katika eneo ambalo linaweza kuleta athari kwenye nyumba yako baadaye.

Na baadhi wamekuwa wakishauri kwamba japokuwa si utaratibu wa watu wengi, lakini ni vyema na kwa usalama wa nyumba, kujenga utaratibu kabla ya kununua kiwanja kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa nyumba, ukawaona wataalamu wakakushauri kama ni salama au la.

Mtaalamu wa shughuli za ujenzi, Victor Mkalama anaeleza athari za kujenga nyumba kwenye kiwanja chenye udongo wa mfinyanzi.

Anasema udongo wa mfinyanzi una tabia ya kuvimba na kuongezeka ukubwa hasa unapopata maji na pia unapokauka husinyaa.

"Kwa maana hiyo udongo unapovimba na kuongezeka ukubwa, jengo hunyanyuliwa juu, lakini udongo unaposinyaa jengo hutitia.

"Kuna aina nyingi za udongo wa mfinyanzi na katika kila aina ya udongo huo hutofautiana na aina nyingine katika kuvimba au kusinyaa na hii inasababishwa na kiasi cha unyevunyevu katika ardhi husika, anasema.

Mtaalamu huyo anasema udongo huo wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo katika eneo husika linalotumika kujenga nyumba inapokatwa.

"Udongo hasa wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo inapokatwa, na hii inatokea kwa sababu mizizi hukomaa zaidi na kunyonya maji kwenye ardhi na kuchangia ongezeko la kiasi fulani cha unyevunyevu kwenye udongo huo.

"Na kuondolewa kwa maji kwenye udondo wa aina hiyo ya mfinyanzi kwa kunyonywa na mizizi ya miti husababisha udongo kuongezeka au kupungua ujazo kwa kiasi fulani hususani katika kipindi cha kiangazi au masika.

"Na kuvimba au kusinyaa huko kwa udongo ni hatari kwa msingi wa nyumba kwa sababu huchangia kuleta nyufa kwenye nyumba na wakati mwingine kuiharibu kabisa."





## Tumia teknolojia kupata kilicho bora

Na Restuta James



TEKNOLOJIA imesaidia mageuzi katika utengenezaji wa samani, kuanzia muundo hadi umaliziaji (finishing), kiasi kwamba hakuna kitu kinachotengenezwa nchi yoyote kisichopatikana hapa nchini.

Hayo ni maneno ya fundi seremala, Ismail Mchambe, anayefurahia ulimwengu wa dijitali, unavyowarahisishia mafundi kubuni kazi mbalimbali za sanaa.

"Uzuri ni kwamba mteja akija na picha ya kiti, meza, kabati au chochote anachotaka, sisi tunakitengeneza. Tunazo samani za nyumbani, ofisini, shuleni, za nje na ndani. Ubunifu unakwenda kasi na sisi tunajitahidi hivyo hivyo," anasema.

Mchambe anasema amekuwa akibuni samani kwa kutumia mbao ngumu, japokuwa hivi sasa matumizi ya mbao laini yameongezeka.

Anasema kinachotofautisha samani za ndani na zile za nje, ni ubora wa mbao ngumu ikilinganishwa na mbao laini zinazotumiwa na mafundi wa nje ya nchi.

Anasema matumizi ya mashine za kisasa unafanya ukamilishaji mzuri wa samani na kwamba kwa mafundi wa nje, mashine zinawapunguzia matumizi ya mbao.

"Sisi bado tunatumia mbao nyingi ndio maana samani zetu ni bora japokuwa mwonekano unaweza usiwe mzuri sana. Za nje mwonekano ni mzuri, ubora ndio changamoto. Sisi tunaona kwamba badala ya kuagiza samani nje, tutafute sample tuwatumie mafundi wa ndani kuzitengeneza kwa mbao ngumu," anafafanua.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
UZURI WA MAPENZI UKIYAHAMISHA TOKA KWA DEMU UKAYAWEKA KWENYE TIMU UNAISHI RAHA MUSTAREHE 'NO VIZINGA'
WE SHUKURU AKILALA NJE ANAKUMBUKA KURUDI KWAKO MMEWE
SIJUI NIMRUKIE KOONI?
JAMANI NIMEOMBA ULINZI WA MBWA SIO 'JIBWA' ONENI SASA! HII NINI SASA?
WOW WOW WOW!
VIBAKA WENGI WANAKULALAMIKIA UNAKUNYWA UBAKIZI HELA MFUKONI ALAFU UNAZURURA USIKU KWANINI?
WAONGO HAWANISACHI KWINGINE
MIMI NI MSHENGA SH'KAMOO
ACHA UCHU! ULIYEMUONA NI MKE WANGU SIO MWANANGU

## HABARI KIMATAIFA

# Biden ahaidi kushinda licha ya umri mkubwa

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amewahakikishia raia wa nchi hiyo kutokuwa na wasiwasi na umri wake na kwamba atashinda nafasi hiyo kwa muhula wa pili.

Akijibu shutuma zinazotolewa kuhusu umri wake kuwa mkubwa kiasi cha kushindwa kuweka sawa kumbukumbu zake, kiongozi huyo alisema yuko vyema kupambana na Donald Trump katika uchaguzi utakaofanyika |Novemba mwaka huu.

Aliwahakikishia wafuasi wake kwamba atashinda tena nafasi ya urais baada ya kutofanya vizuri katika mdahalo wa urais ulioibua wasiwasi kuhusu hali yake.

"Najua mimi si kijana, kusema kweli," alisema katika mkutano alioufanya jana North Carolina.

Kauli hiyo aliitoa siku mbili baada ya kuhangaika katika mpambano wa mdahalo katika televisheni na mpinzani wake kutoka chama cha Republican, Donald Trump.

"Sitembei kirahisi kama nilivyokuwa zamani. Sijadili kama nilivyokuwa nikijadili. Lakini ninachojua, kwa hakika, najua jinsi ya kufanya kazi hii." Alisema huku akishangiliwa na wafuasi wake.

Rais Biden, mwenye miaka 81, alisema anaamini kwa moyo mmoja kwamba angeweza kuhudumu muhula mwingine, huku umati wa watu waliokuwa wakishangilia mjini Raleigh wakisema kwa sauti "miaka minne mingine".

Wakati huo huo, Trump alifanya mkutano wa kampeni wa aina yake huko Virginia, na alisifia ushindi wake alioupata katika mjadala huo, ambao CNN ilisema ulitazamwa na watu milioni 48 kwenye televisheni na mamilioni zaidi mtandaoni.

"Tatizo la Joe Biden sio umri wake, ni uwezo wake. Hana uwezo kabisa," alisema Trump.

Rais huyo wa zamani alisema haamini uvumi kwamba Biden angejiondoa katika kinyang'anyiro hicho, akisema anafanya vyema zaidi katika uchaguzi kuliko wagombea wengine wa Democratic, akiwemo Gavana wa California Gavin Newsom na Makamu wa Rais Kamala Harris.

**BBC.**



Raia wa Mauritania wakishiriki zoezi la upigaji kura jana, jumla ya watu milioni tano walipiga kura kumchagua rais. **PICHA: AFP**

# Mauritania wapiga kura kumchagua rais wao

**NOUAKCHOTT,** MAURITANIA

RAIA wa Mauritania wamepiga kura katika uchaguzi mkuu ambao rais aliyeko madarakani Mohamed Ould Ghazouani, anachuana na wagombea sita wa upinzani. Ghazouani, (67), ambaye ni mwanajeshi wa zamani wa ngazi ya juu, ameahidi kuharakisha uwekezaji ili kuchochea uongezeko la uchumi na mahitaji ya bidhaa muhimu.

Nchi hiyo yenye watu milioni tano, wengi wao wanaishi katika umaskini licha kuwa na utajiri mafuta na madini.

Rais Ghazouani ambaye alichaguliwa muhula wa kwanza mwaka wa 2019, anatarajiwa kushinda uchaguzi kutokana na umaarufu wa chama tawala. Wapinzani wake ni mwanaharakati anayepinga utumwa Biram Dah Abeid, mwanasheria Id Mohameden M'Bareck, mchumi Mohamed Lemine El Mourtaji El Wafi na Hamadi Sidi El Mokhtar wa chama cha Tewassol.

**DW**

# Wanajeshi kuendelea kuilinda mitaa Kenya

**NAIROBI,** KENYA

SERIKALI ya Kenya, imesema jeshi la nchi hiyo litaendelea kushika doria mitaani hadi hali ya kawaida itakaporejea.

Hatua hiyo imekuja baada ya wiki moja ya machafuko ya kisiasa yaliyotokana na maandamano yaliyofanywa na vijana wanaojiita Gen-Z kupinga mswada wa fedha wa 2024.

Hata hivyo, nchi hiyo inajiandaa kwa duru mpya ya maandamano yatakayofanyika wiki ijayo, kuendeleza maandamano yaliyomlazimu Rais William Ruto kusitisha kusaini mswada huo.

Muda mfupi baada ya jaji kuamuru vikosi vya usalama kutotumia nguvu kupita kiasi dhidi ya waandamanaji, Waziri wa Ulinzi wa Kenya, Aden Duale, alitangaza kwamba jeshi litaendelea kusaidia polisi ambao walikuwa wamezidiwa na waandamanaji.

Duale alisema hatua hiyo ni ya dharura ya usalama iliyosababishwa na maandamano ambayo yaligeuka kuwa ya vurugu.

Kulingana na shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch, takribani watu 30 waliuawa wakati polisi waliowafyatulia risasi waandamanaji.

Shirika hilo linadai kuwa vikosi vya usalama vililenga waandamanaji waliokuwa wakijaribu kukimbia.

Vijana hao waandamanaji wanataka kuondolewa kazini watu waliopewa kinyume na katiba, kuondolewa kwa kodi zingine, na kufutwa kazi kwa watumishi wa serikali wenye uhalifu.

**BBC**

# Uchaguzi Iran kurudiwa Julai

**TEHRAN,** IRAN

TUME ya uchaguzi ya Iran imetangaza kuwa wagombea wawili Masoud Pezeshkian mwenye msimamo wa kati na mhafidhina Saeed Jalili watakwenda katika duru ya pili ya uchaguzi wa urais wa taifa hilo.

Pezeshkian alipata karibu asilimia 42.5 ya kura na Jalili akafuata kwa asilimia 38.7. Lakini kuna wagombea wengine wawili katika kinyang'anyiro hicho ambao walipata asilimia za chini.

Kwa kuwa hakuna aliyepata idadi kubwa ya kura kumfanya aunde serikali, tume ilitangaza kurudiwa kwa uchaguzi Julai 5, mwaka huu.

Takriban wapiga kura milioni 61 nchini humo walipiga kura Ijumaa kumchagua mrithi wa Ebrahim Raisi, ambaye alifariki katika ajali ya helikopta mwezi Mei.

**DW**

# Waasi M23 wauteka mji mwingine DRC

**GOMA,** DRC

WAASI wa kundi la M23 wameuteka mji wa kimkakati wa Kanyabayonga ulioko mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo baada ya mapigano makali na vikosi vya serikali.

Waasi hao walichukua udhibiti wa maeneo mawili kabla ya kuuteka Kanyabayonga jana. Mji huo muhimu ulioko kati ya vituo vikuu vya kibiashara vya Butembo na Beni kaskazini mwa nchi hiyo.

Ofisa mmoja wa eneo hilo aliripoti kuwa wakazi walikimbia makazi yao majira ya alfajiri wakati waasi walipoanzisha mashambulizi.

Kanyabayonga umekuwa kimbilio la maelfu ya watu ambao wametoka katika maeneo yaliyochukuliwa na waasi katika miezi ya hivi karibuni.

Mkoa wa Kivu Kaskazini umekumbwa na ghasia tangu 2021, wakati M23 walipoanzisha tena mashambulizi yao.

Hata hivyo, DRC imefuta mazungumzo yoyote na M23.

DRC na Umoja wa Mataifa, inaishutumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi, madai ambayo nchi hiyo inakanusha.

**BBC**

SAFU

MAKALA

# TUKIBADILIKA KIFIKRA, TUTABADILISHA MAISHA YETU



Na Magabilo Masambu

Dhana ya pili ambayo ndiyo muhimu zaidi kuliko ya kupata ajira ni kutoa ujinga, ujinga ukishatoka utakuwa na akili ya kufanya na mengine ambayo hukusomea.

MABADILIKO yoyote tunayoyaona yakitokea duniani tutakubaliana kwamba yanatokana na mtazamo wa kifikra. Kwa maana nyingine ni kwamba, tukitaka kubadili maisha yetu lazima tubadili kwanza namna ya kufikiri. Dunia inabadilika tusipobadilika sisi wenyewe itatubadilisha bila kupenda.

Kwa sasa bado kuna hii dhana kwamba watu waliosoma hawapaswi kufanya shughuli nyinginezo tofauti na fani zao walizozisomea. Mara kadhaa imesikika ikisemwa na watu kwamba, yule au huyu ana shahada ya kitu fulani lakini ni mchekeshaji, bodaboda, mkaanga chips na kadhalika.

Hali hii inaonesha wazi kwamba, pamoja na dunia kubadilika, sisi bado tungali na mawazo yaleyale ya kudhani elimu ni njia pekee ya kufanikiwa.

Ni kweli kwamba elimu ya mzungu ni mfumo unaowaandaa watu kuwa mameneja, wasimamizi wa kazi na kwa sehemu wafanyakazi, lakini kama hakuna cha kusimamia au cha kufanya kwanini tuendelee kuiamini kama njia pekee ya kutufanya tufanikiwe?

Dhana ya pili ambayo ndiyo muhimu zaidi kuliko ya kupata ajira ni kutoa ujinga, ujinga ukishatoka utakuwa na akili ya kufanya na mengine ambayo hukusomea. Tabia ya kuendelea kuwashangaa waliofika vyuo vikuu kufanya kazi nje ya taaluma zao ni kuendelea kuwafanya vijana wengi waendelee kusubiri kupata ajira ambazo kimsingi zimeshakuwa tabu, badala ya kutumia vipawa vingine walivyopewa na Mwenyezi Mungu ili waishi.

Ni jambo halikuzoeleka huko nyuma kumwona mwanamke anaendesha daladala, lakini sasa tunapaswa kuzoea na kuona ni kitu cha kawaida kwa sababu dunia ya leo si ile ya jana. Baadhi ya jamii zilishabadilika muda mrefu kidogo.

Wakati fulani nilikuwa ninafundisha 'twisheni' ya somo la Fizikia mahali fulani, nikapata wanafunzi watatu kutoka familia ya raia Mtanzania mwenye asili ya India. Baada ya kufundisha watoto hao kwa siku tatu hivi, nikaanza kuona wazazi wa watoto hao wanakuja kukaa darasani kuona ninawafundisha nini watoto wao.

Kitu ambacho sikujua ni kwamba, kumbe kila walipotoka kusoma walipelekwa dukani kupimwa ikiwa wanaweza kuuza bidhaa na kurudisha 'chenji' kwa wateja. Bahati mbaya wakashindwa kurudisha 'chenji', kwahiyo wale wazazi wakaona hakuna uhalisia kati ya kufundishwa Fizikia na kurudisha 'chenji'.

Yaani fikra zao si kutaka mtoto asome ili baadaye akatafute kazi mahali, wanataka akishasoma vizuri auze duka la nyumbani.

Uhaba wa ajira limekuwa tatizo la dunia, hata huku kujiajiri nako itafika mahala patajaa, tunaweza kuona kama mfano tu suala la uchekeshaji, lilianza na watu wachache japo walishaanza kitambo kina Mr Bean, msomi wa hesabu na kemia huyu, kwa hapa kwetu tutakumbuka kundi la The Comedy la kina Masanja Mkandamizaji.

Hivi sasa uchekeshaji ni ajira rasmi ya vijana wengi na inakusanya watu wengi.

Yote haya ni kujaribu kujitafutia riziki na hapa ndipo linapokuja suala la kutotaka kutumia elimu zetu tena, hata kama tunazo kubwa kutafuta ajira badala yake kutumia vipaji kutafuta maisha.

Zamani wakati nchi inapata uhuru, watu walikuwa wakiulizwa, tukupatie kazi gani? Dunia ya leo inataka unajua nini? Si una elimu kiwango gani, kwa sababu kama ni elimu tu wapo wengi wenye elimu kama yako au zaidi.

Kwahiyo, elimu ikitumika kama kigezo pengine utakosa kazi, lakini unachofahamu hakiwezi kuwa mbadala wa mwingine, ndiyo maana unaweza kuwa na wachekeshaji wawili kwenye jukwaa moja na ukawafurahia wote, kwa sababu kwenye kufahamu kitu kila mmoja anakuwa na upekee wake.

Ushauri wangu; elimu yako isiwe kifungo, fanya chochote, mradi huvunji sheria ya nchi na wala hauvunji maadili yetu kama Watanzania na Waafrika ili uweze kupata kula yako ya kila siku, ukijiona umesoma, wako waliyosoma zaidi yako na wametulia tu, wanafanya makubwa yasiyoendana na taaluma zao.

Mtazamo wa jamii ubadilike, dunia imebadilika, walioimba muziki wakaonekana wahuni leo ni mawaziri na wakuu wa wilaya.

**magabilomjalifu@gmail.com**
**0689157789**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Baba aliyehama mtaa uswazi kukimbia milio ya paka usiku*



Na Adam Fungamwango

Hizi ni dhana ambazo zimekuwepo enzi na enzi, na zimekuwa zikirithishwa, lakini mpaka sasa wanasayansi hawajathibitisha usahihi na jambo hilo ambalo linabakia kuwa ni imani na dhana tu.

JAMII ya Kifrika hadi leo wapo wanaoamini kuwa ukikutana na baadhi ya wanyama, ndege au kusikia milio yao basi ni mikosi.

Imani hizi za tangu zama hizo zimekuwa zikirithishwa vizazi na vizazi.

Licha ya kuwa dunia kuwa na maendeleo makubwa ya teknolojia na elimu, lakini bado kuna waliobaki na misimamo yao ile ile ya imani hizo.

Mmoja wa wanyama ambao wanatajwa kuwa wakilia usiku ni matatizo na mkosi mkubwa ni paka.

Baadhi wanaamini aina yao ya milio isiyokuwa ya kawaida inaweza kusababisha matatizo, mmoja kati ya watu au familia zinazozunguka eneo hilo anaweza kupatwa na kitu chochote kibaya, kama vile ajali, au kifo kutokea.

Inapotokea kama kuna mgonjwa ndiyo kabisa, imani yao kuwa atafariki dunia.

Katika ndege wote, bundi naye ana bahati mbaya. Walie ndege wote, lakini bundi sauti yake ikisikika basi itafsiriwa ni mkosi.

Kama kuna mgonjwa basi watu wanakaa tayari kupokea chochote kitakachotokea.

Hizi ni dhana ambazo zimekuwepo enzi na enzi, na zimekuwa zikirithishwa, lakini mpaka sasa wanasayansi hawajathibitisha usahihi na jambo hilo ambalo linabakia kuwa ni imani na dhana tu.

Bara la Afrika linadaiwa kuwa na tamaduni nzuri zaidi kuliko mengine, na kwa kiasi kikubwa zinafanana, kama vile kuheshiana, mdogo kumheshimu mkubwa na mkubwa kumjali mdogo.

Hata hivyo kuna imani au tamaduni chache zimekuwa changamoto kubwa, na zimeshaanza kupigwa vita, ikiwemo kukeketa wanawake na nyingine zinazoonekana kwa dinia ya sasa hazifai.

Tukirudi kwenye imani zetu ambapo ikitokea sehemu paka wanalia sana usiku watu wanakuwa na hofu kwao wenyewe na familia zao.

Kwa sababu wanamuziki na wasanii ni kioo cha jamii, wanatunga nyimbo kutokana na kile kile kinachoonekana au kutokea ndani yake.

Ukikitazama kioo ujue wewe ndivyo ulivyo.

Huwezi ukakikasirikia kioo kusema sivyo ulivyo. Wanachoimba wanamuziki hasa wale wa zamani mara nyingi kinakuwa kimewapata wao wenyewe, familia zao, ndugu, majirani zao, rafiki au wapenzi wao.

Mwaka 1978, Mbaraka Mwinshehe Mwaruka, akiwa bendi yake ya Super Volcano, alifyatua kibao kimoja kilichobeba dhana ya ushirikina, kiitwacho, 'Mtaa wa Saba.'

Wimbo huu umebeba dhana za Waafrika wengi kuhusu ushirikina na wanyama wanaodaiwa kuwa wakilia ni uchuro na kitu kibaya kitatokea.

Maudhui ya wimbo huu ni kwamba baba mmoja aliyekuwa akikaa nyumba ya kupanga ambayo haikuwa na riziki, badala yake mikosi kila siku, lakini alipohama kwenda kukaa mtaa wa mbali na hapo, mambo yake yalianza kunyookea.

"Sasa nimehamia mtaa wa saba, toka pale nilipokuwa nikikaa zamani, ile nyumba siyo nyumba ilikuwa na mikosi.

Sasa nimehamia mtaa wa saba, toka pale nilipokuwa nikikaa zamani, ile nyumba siyo nyumba ilikuwa na mikosi.

Nimehama nimehama kuona balaa imezidi, na mdomo haushi ndani ya nyumba yooo jama, ndoto ndoto za ajabu haziishi tulalapo.

Darini hakusemeki mapaka hayaishi kulialia, usiku kucha usingizi hauji kabisa, watoto hawaishi kuumwaumwa, eee jamaa."

Hapa jamaa anaelezea mambo yaliyokuwa yamempata katika nyumba aliyokuwa akiishi awali, anakwambia huwa anaota mpaka ndoto za jinamizi.

"Maneno maneno hakuna, tunaishi kwa raha sana, wapangaji hawana zogo nami, baba mwenye nyumba sina madhila naye nashukuru Mungu yeyeye.

Na sioti ndoto mbaya, hata mwezi sijamaliza kazini wakanipandisha na cheo na mama yao sasa kuumwaumwa kote kumekwisha yeyeye.

Maneno maneno hakuna, tunaishi kwa raha sana, wapangaji hawana zogo nami, baba mwenye nyumba sina madhila naye nashukuru Mungu yeyeye.

Na sioti ndoto mbaya, hata mwezi sijamaliza kazini wakanipandisha na cheo na mama yao sasa kuumwaumwa kote kumekwisha yeyeye."

Jamaa amehamia mtaa wa saba kila kitu kinakwenda poa, watoto na mama hawaumwi, na kazini amepandishwa cheo. Imani yake inamwambia kuwa kila kitu kimekaa sawa baada ya kuhama kule alikokuwa mwanzo.

Hizo ndizo dhana za baadhi ya Waafrika ambazo wanaamini. Siyo kipindi cha kina Mbaraka tu, bali hadi leo hii.

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MZEE sijui niseme nini. Hili jambo limenitesa kwa muda mrefu, familia yangu hasa shangazi yangu. Amehangaika sana. Amepoteza pesa nyingi sana. Shangazi yangu ni masikini sana, wakati mwingine hata kula yetu ni ya shida, lakini alipambana mpaka akashindwa. Leo hii ni kama ndoto kwangu, nimepona kirahisi sana. Naamini nimepona kwa sababu haijawahi kutokea nikakaa dakika zote hizi bila kupandisha. Mimi ilikuwa ikinipata harufu ya manukato tu, hasa udi, napandisha hapo hapo, muulize Heri atakuambia. Sijui nikupe zawadi gani mzee, ila naomba uwe kama mzazi wangu kuanzia leo."

"Nilikuambia binti yangu siku ile kuwa nitakusaidia bure. Na hii ni kwa sababu ya huyu mwenzako. Ni rafiki yangu sana na yeye hakuona mtu mwingine wa kumsaidia akanitafuta. Wala halina tatizo, wewe na huyu mwenzako, wote ni kama wanangu tu.

Na kwa hili nadhani tutakuwa karibu sana. Nahitaji pia kumuona huyu shangazi yako." "Yaani baba, nikirudi na kumwambia hili sijui atacheza ngoma gani. Sijui atapika chakula gani shangazi yangu jamani. Ila nakuomba jambo moja mzee wangu kama hutojali." "Jambo gani hilo mwanangu?" Mzee raia akauliza. Nuru akaangua kicheko kilichowashangaza wote. Hawakujua kwa nini anacheka.

"Jambo ninaloomba umelijibu mwenyewe." "Nimelijibu?" Akashangaa. "Ndiyo umetamka mwenyewe mwanangu! Nataka uwe baba yangu. Baba yangu wa hiari, wa damu kuanzia leo." Mzee Raia alimtazama Heri kana kwamba yeye ndiyo aliumuomba. "Baba yako peke yako, na mimi pia." Heri akadakia.

Mzee raia alichokishuhudia ni furaha iliyowazidi vijana wale. Wakamshika Heri kwenye mkono wake wa kulia, na kushoto akamkamata Nuru, na kuwavuta pamoja pale alipokuwa yeye.

"Wote ninyi mtakuwa wanangu, na ombi hilo limelikubaliwa kwa mikono miwili." Heri na Nuru walirukaruka kwa furaha kwa nusu furaha, nusu mzaha, hatimaye wakakumbatiana, wakimjumlisha mzee Raia.

Ni siku ambayo mzee Raia alijawa na furaha sana. Alijiona kama amerejea kuwa kijana ghafla. Akajawa na amani ya moyo.

Hakuwahi kushangiliwa na kuthaminiwa na mtu yeyote yule




**Wakaendelea na furaha yao, wakarukaruka na kumzunguka mzee Raia kwa namna ya utani, ghafla tu wakaanza kuimba "Baba baba baba..."**

hata watoto wake wa kuwazaa kama vijana hao. Machozi ya furaha yalimtoka babu wa watu. "Nitahakikisha mnaoana." Maneno hayo yalimtoka tu bila hata kuwaza aseme nini. Vijana wale walishangilia kama vile wanaotazama mpira wanavyofanya goli likiingia.

Wakaendelea na furaha yao, wakarukaruka na kumzunguka mzee Raia kwa namna ya utani, ghafla tu wakaanza kuimba "Baba baba baba..."

Furaha yao ilishika kwa mzee Raia kufanya maombi na sala ili si tu kuwafanya wote wawe na afya njema, lakini vijana hao wafanikiwe katika maisha yao watakayoyatengeza baadaye kuwa hawapo vizuri sana kichumi.

***************************

Shangazi yake Nuru hakuamini alichokuwa akikisikia. Amehangaika kwa miaka yote kumtibu binti yake lakini imeshindikana .

Akapoteza pesa nyingi, hizo hizo anazodunduliza kwa biashara yake ya kukaanga mihogo.

Na mara kwa mara alikuwa akiishiwa msingi na kulazimika wakati mwingine kukaa wiki mbili bila kufanya biashara, akitafuta msingi huku na huko, ilifika wakati mpaka akaingia kwenye mikopo ya kinyonyaji maarufu kama kausha damu.

Leo hii mtoto wa marehemu kaka yake amepona. Amepona kirahisi sana kuliko ilivyodhaniwa. Ameponyeshwa bure bila ya kulazimika kutoa hata shilingi moja.

Awali hakuamini. Alikwenda kununua pafyumu moja ndogo kali ambayo aliamini ingenuswa kwenye pua za Nuru, angepandisha. Aliacha kuitumia miaka mingi iliyopita kutokana na kuwa mara kwa mara akipandisha maruhani anapoipata harufu yake.

Alipohakikisha na kuamini kuwa sasa Nuru hana tena maruhani, alipiga yowe na vigelegele. Akazunguka varanda nzima, na baada ya hapo akaanza kuimba wimbo wa lugha ya kwao.

Muda wote huo, Heri aliyekuwa amekaa kochi moja na Nuru, huku mzee Raia akiwa katika kochi lingine walimtazama kwa tabasamu na vicheko.

"Nawashukuru sana. Yaani sujui niseme nini. Sijui nifanye nini. Nakushuru sana mzee, nakushukuru sana kijana. Ni vijana wachache sana wenye moyo kama wako.

Binti yangu amenisimulia yote yaliyotokea huko kwenu. Ingekuwa mtu mwingine angemfukuza. Na hata kama isingekuwa hivyo, angemuacha aondoke na asingemtafuta tena, urafiki ingekuwa imeisha. Baadhi ya wanaume wanapenda wanawake wakiwa wazima wa afya. Ikitokea changamoto kidogo tu, hawawezi kukabiliana nazo na kuwasaidia.

Wewe umefanya hivyo. Na ndiyo umefanikisha kwa kiasi kikubwa kuhakikisha Nuru anapata matibabu. Na kweli leo mzima, amepona," maneno yalimtoka shangazi yake Nuru kama mtu anayeomboleza. Yalikuwa yamechanganyika na furaha pamoja na huzuni.

"Kaka yangu!" Akageukia mzee Raia. "Yaani sijui nikushukuru vipi. Umemfanya binti yangu awe huru. Alikuwa kwenye kifungo! Alikuwa ametupiwa jini lililokaa mwilini mwake na mama yake ya kambo, ili tu asiolewe. Leo umepambana na limetoka, umefanya hivyo bure tu, wakati mimi nimetupa pesa nyingi sana bila mafanikio. Naweza kusema huyu binti sasa, ambaye hana baba wala mama, siyo wa kwangu peke yangu sasa. Ni wenu pia. Kama mmeweza kumuondoa kwenye minyororo hiyo, basi sidhani kama mnaweza kumtupa tena..." Hakumalizia na kuanza kulia.

Ilianza kazi ya kumbembeleza na kumtuliza. "Na sisi tumefanya hivi kwa sababu tunamhitaji binti yako. Huyu hapa amefika. Tayari mimi nimeshakuwa baba yake ya hiari. Nina nyumba yangu nyingine Gongolamboto, nataka nitoe vyumba viwili na varanda kwa ajili ya binti huyu akakae bure kabisa, tena nitafanya kwa maandishi, hata nikianguka leo hakuna mtu wa kuwatoa mpaka watakaamua kuondoka wenyewe." Mzee Raia akaleta habari mpya kabisa. "Sasa Mzee Raia, unaposema umempa Nuru, halafu hapo hapo unasema watakwenda kukaa, huyo mtu atakayekwenda kukaa naye ni na nani?" Swali hilo liliwavunja mbavu wote.

"Atachagua mwenyewe binti yangu wa kukaa naye!" Akajibu mzee Raia kimzaha. "Eti Nuru unataka kwenda kuishi na nani Gongolamboto?" Nuru alitabasamu, halafu akaangua kicheko "Heri" Akatamka na kuonekana kama ana aibu hivi.

Heri akamfuata na kumkumbatia Nuru. "Shangazi, tangu leo ujue mimi ndiyo nitakuwa na Nuru, nampenda sana huyu binti. Yote niliyofanya kwa ajili yake ni kwa sababu nampenda. Kifupi tu ni kwamba nitamuoa na taratibu zote nitazifanya upesi, ili zikamilike."

"Basi umeshajijibu mwenyewe, hiyo nyumba mtaenda kuishi wote, na nilijua tu utamuoa, na wakati nafikiria hilo nilijua nyinyi wawili ndiyo mtakaoishi pale." Alisema mzee Raia.

"Mimi sina tatizo la kuolewa Heri, ila jini Anzura umeshawasiliana nalo ili likuruhusu unioe?"

"Hana lolote, safari hii likija litajua mimi ni nani!"

"Mhh!!! Siku ile umelikimbia, ukaliachia chumba."

"Nishalijua ujanja wake, lenyewe ndiyo limekimbia sasa." Yalikuwa ni majibizano ya utani, masihara na mzaha baina ya wapenzi hao wawili waliokuwa wamekumbatiana, pembeni yao shangazi na mzee Raia walikuwa wakiwaangalia kwa furaha na vicheko.

**MWISHO**



# MAN FONGO ANAKUJA HIVI....

MKALI wa Singeli nchini Man Fongo, amesema yuko mbioni kutoa ngoma mpya hivi karibuni ambayo atamshirikisha msanii maarufu.

Man Fongo ambaye sasa yuko nje ya nchi, amesema kolabo hiyo ikikamilika atafanya ngoma nyingine na wasanii wa nje ya nchi ambao hakuwataja.

"Nikirudi Tanzania nataka niachie goma jipya ila sasa hilo goma nataka liwe kolabo na msanii wa hapo nyumbani kabla sijaachia kolabo zangu na wasanii wa nje ya Tanzania," ameandika Man Fongo katika ukurasa wake wa Instagram.

# TANASHA AKUBALI MATOKEO

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Tanasha Donna, amesitisha utambulisho wa ngoma yake mpya kutokana na vurugu zinazoendelea nchini humo.

Kupitia mtandao wake wa Instagram, Tanasha amewaambia mashabiki wake kwamba alikuwa ameweka kila kitu tayari kutambulisha Ijumaa iliyopita, lakini ameahirisha ili kuomboleza watu waliokufa katika maandamano yaliyofanyika wiki hii.

"Single yangu ya kwanza kutoka kwa project yangu ilikuwa itoke leo, lakini tunaomboleza vifo vya mashujaa wetu wachanga, hadi badae," amesema Donna.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAMKOMALIA PALHINHA
BAYERN Munich imewasilisha ofa ya mwisho kwa Fulham ya thamani ya pauni milioni 38 ili kumsajili kiungo wa Ureno mwenye umri wa miaka 28, Joao Palhinha, ambaye tayari ameshafikia makubaliano ya awali na klabu hiyo ya Ujerumani. (**Sky Sports Germany**)

### KILMAN KUTUA WEST HAM
WEST Ham iko tayari kutoa pauni milioni 35 ili kumnasa beki wa Wolves ambaye ni raia wa England, Max Kilman, lakini pia wako tayari kusaka mabeki wengine wa kati endapo klabu hiyo ya Midlands itashikilia msimamo wake wa kulipwa pauni milioni 45 ili kumuuza nyota huyo mwenye miaka 27. (**Guardian**)

### CHELSEA KUMUUZA LUKAKU
CHELSEA inasisitiza inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 37 ili kumuuza straika wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, ingawa AC Milan na Napoli zinatarajia dau na nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 litashuka majira ya joto. (**Gianluca di Marzio**)

### BARCELONA, PSG VITANI
BARCELONA na Paris St-Germain wanatarajia kumshawishi mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Julian Alvarez mwenye umri wa miaka 24, kuondoka Manchester City. (**Caught Offside**)

### ABRAHAM ATAJWA MILAN
AC Milan wameonyesha nia ya kumsajili straika raia wa Englland, Tammy Abraham (26), ambaye mkataba wake na Roma ya Italia utamalizika ifikapo 2026. (**La Gazzetta dello Sport - in Italian**)

### ZIRKZEE ANUKIA UNITED
MANCHESTER United inatazamia kukidhi kipengele cha kuachiliwa kwa Joshua Zirkzee huku wakipanga kumuuza Mason Greenwood ili kufadhili mpango huo, nao Everton wakitakiwa kuwasilisha ombi jingine kwa Jarrad Branthwaite.(**Mail**)

### BRANTHWAITE SOKONI EPL
KLABU ya Everton inatarajia Manchester United itawasilisha ofa nyingine kwa beki wa Timu wa Taifa wa England, Jarrad Branthwaite, mwenye umri wa miaka 21. (**Liverpool Echo**)

### NDIAYE KUTUA EVERTON
EVERTON inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Senegal, Iliman Ndiaye, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Marseille ya Ufaransa. (**Footmercato**)

### TEN HAG, UNITED KUTETA
MANCHESTER United inatarajia kukubaliana mkataba mpya na Kocha, Erik ten Hag, kabla ya kuanza kwa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani mwezi ujao. (**ESPN**)

### NISTERLROOY KUMSAIDIA HAG
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy mwenye umri wa miaka 47, amefanya mazungumzo chanya kuhusu kurejea katika klabu hiyo kama sehemu ya wasaidizi wa Erik Ten Hag. (**Talksport**)

### JOSELU KUONDOKA MADRID
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Joselu, mwenye umri wa miaka 34, anakaribia kuondoka Real Madrid baada ya kupokea ofa kutoka kwa klabu ya Qatar Al Gharafa. (**Athletic**)

### CHELSEA, BARCA KUKUTANA
CHELSEA imeanza mazungumzo na Barcelona kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wa Hispania, Marc Guiu, mwenye umri wa miaka 18. (**ESPN**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KOCHA BRAZIL AMVULIA 'KOFIA' VINÍCIUS JÚNIOR

**LAS VEGAS,** Marekani

## Ni baada ya kuonyesha kiwango bora huku akifunga...

KOCHA wa Brazil, Dorival Júnior, alimpongeza Vinícius Júnior baada ya fowadi huyo kufunga mabao mawili na kuwasaidia Seleção kurejea katika mstari wa Copa América kwa kumaliza na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Paraguay huko Las Vegas juzi.

**Brazil na Vinícius walitatizika katika mchezo wa ufunguzi wa mashindano hayo kwa kutoka suluhu na Costa Rica, ambapo nyota huyo wa Real Madrid alishindwa kupiga shuti langoni na akatolewa katikati ya kipindi cha pili.**

Lakini alikiwasha tangu mwanzo dhidi ya Paraguay, na kuiweka Brazil mbele baada ya dakika 35 kwa kumalizia pasi ya Lucas Paquetá.

Baada ya Sávio kufanya mambo kuwa 2-0, Vinícius aliipatia Brazil bao la tatu kabla ya kipindi cha mapumziko alipompita beki wa Paraguay Omar Alderrete na kujaribu kuuweka mpira wavuni.

Vinícius angeweza kufunga hat-trick lakini badala yake aliamua kumpasia Paqueta, ambaye alikosa nafasi katika kipindi cha kwanza, kuongeza kasi na kufunga penalti kipindi cha pili.

"Leo (juzi), alicheza mechi vizuri sana kabisa," Dorival alisema kuhusu Vinícius.

"Siku zote mimi husema sichezi mwenyewe nacheza kitimu," alisema Vinícius katika mahojiano ya uwanjani kufuatia mchezo huo.

"Ninapochezea Brazil ninaichezea nchi yangu, huwa najaribu kufanya mambo mazuri zaidi lakini haiwezekani kila mara.

Ushindi huo ulikuwa jibu kamili kutoka kwa Brazil baada ya kuanza kwa mchujo nchini Marekani na kuwaweka washindi hao mara tisa kwenye hatihati ya kutinga robo fainali.

Ikiwa na pointi nne, Brazil iko pointi mbili nyuma ya kinara wa kundi lao, Colombia ambayo iliifunga Costa Rica mabao 3-0 katika mechi ya mapema hapo juzi.

Ushindi au sare ya Brazil dhidi ya Colombia Jumanne iliyopita unahakikisha moja ya nafasi mbili za kundi hilo katika hatua ya mtoano.

Brazil pia ina faida ya tofauti ya mabao sita dhidi ya Costa Rica, kwa hiyo kupoteza kunaweza kuwazuia mabingwa hao mara tisa wa Copa América.

# BELLINGHAM ASHUKIWA ENGLAND



**BERLIN,** England

JUDE Bellingham amekuwa mmoja ya wahanga wa mashabiki wa soka wa England na ulimwenguni kwa ujumla baada ya kuonyesha kiwango kisichoridhisha katika michuano ya Euro 2024 hadi sasa.

Licha ya kuongoza katika michuano ya Euro 2024, England imezidi kuleta wasiwasi kutokana na kiwango kibovu katika michezo yao yote ya hatua ya makundi.

England imeshinda mchezo mmoja tu tena kwa goli moja, halafu ikatoa sare katika michezo miwili iliyofuata na kumaliza kileleni mwa kundi hilo wakiwa na jumla ya pointi tano.

Viwango vya wachezaji kadhaa wakiwamo Trent Alexander Arnold, Bukayo Saka, Phil Foden, Kyle Walker, Declan Rice na Bellingham vimekuwa vikikosolewa na mashabiki pamoja na wachambuzi mbalimbali.

Katika mchezo dhidi ya Slovenia, Bellingham hakupiga shuti wala kutengeneza nafasi yoyote.

Pia hakufanya yoyote wala hakupiga krosi iliyofika. Katika hayo pia, Bellingham alipoteza mipira mara 15, hali iliyozua mijadala katika mitandao ya kijamii kwani hata katika mchezo wao wa pili dhidi ya Denmark, Bellingham hakupiga shuti lolote.

# Yamal afaulu mtihani wa mwisho



**BARCELONA,** Hispania

WINGA wa Barcelona, Lamine Yamal, anasherehekea kabla ya mechi ya hatua ya 16 bora ya Euro 2024 kati ya Hispania dhidi ya Georgia itakayochezwa leo baada ya kufaulu mitihani yake ya shule.

Yamel mwenye umri 16, alipokea habari njema katika kambi ya Hispania ya mazoezi kusini mwa Ujerumani, ambapo amekuwa akichanganya elimu yake na kuiwakilisha nchi kwenye mashindano hayo.

"Nimetoka tu mazoezini na nimeambiwa yote yalikwenda vizuri," Yamal alikiambia kituo cha redio cha Hispania Onda Cero. "Nimefaulu mitihani na nina sifa sasa.

"Kama ni kweli, niliwaona kwenye simu yangu na ilisema nimepita kwa hivyo nilifunga tu maombi, nikampigia mama yangu na kumwambia."

Matokeo yanalingana na mwaka wa nne wa ESO, ambayo ni hatua ya mwisho ya elimu ya sekondari Hispania, takribani sawa na mitihani ya GCSE ya Uingereza au diploma ya shule ya sekondari nchini Marekani.

Yamal, ambaye atatimiza umri wa miaka 17 siku moja kabla ya fainali ya Euro 2024, alikuwa amefichua mapema katika michuano hiyo alileta kazi yake ya nyumbani kwenye michuano ya Euro.

# Pepe : Ronaldo anaishi kwa kupachika mabao

**BERLIN,** Ujerumani

MLINZI wa Ureno, Pepe, amepongeza matokeo chanya aliyonayo Cristiano Ronaldo katika timu ya taifa licha ya mshambuliaji huyo mahiri bado hajafunga bao katika michuano ya Euro 2024, inayoendelea.

Ronaldo, ambaye anacheza katika rekodi ya sita ya michuano ya Ulaya, ameanza kwenye michezo yote mitatu ya Ureno huko Ujerumani.

"Cristiano anaishi kwa mabao, huo ni ukweli," alisema Pepe katika mkutano wa wanahabari hapo juzi.

"Lakini umeona uwepo wake uwanjani kusaidia timu ya taifa? Inashangaza. Ni mchezaji mwenye dakika nyingi zaidi katika timu yetu, akiwa na umri wa miaka 39."

Ureno walishinda michezo yao miwili ya ufunguzi lakini wakapata kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Georgia katika mchezo wao wa mwisho wa hatua ya makundi.

"Tulijua safari hii haingekuwa rahisi, haijalishi ni wangapi kati yenu mlisema tayari imeshinda," Pepe alisema.

"Sio hivyo na tulijua. Ni lazima ucheze dakika 90 na, ikibidi dakika 120. Tunataka kufanya kazi nzuri kwa ajili ya nchi yetu na ndivyo tutakavyofanya katika mchezo ujao."

Ronaldo, ambaye alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Euro 2020 baada ya kumaliza kama mfungaji bora akiwa na mabao matano, aliingia kwenye michuano ya majira ya kiangazi akiwa ameifungia a mabao 35 Al Nassr ya Saudi Arabia.

Pia alijifua kwa ajili ya Euro 2024 kwa kufunga mabao mawili katika ushindi wa 3-0 wa Ureno dhidi ya Jamhuri ya Ireland mnamo Juni 11, mwaka huu na kuongeza rekodi yake ya kimataifa kwa wanaume hadi kufikia magoli 130.



# JKT TANZANIA YAJIPANGA KUMPA UNAHODHA BOCCO

**Na Adam Fungamwango**

KAMA mambo yataenda kama yalivyopangwa, JKT Tanzania itamtangaza straika mkongwe nchini, John Bocco, kuwa mchezaji na nahodha wa timu hiyo kuelekea msimu mpya wa mashindano wa mwaka 2024/2025.

Habari zilizopatikana jana kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema, licha ya nahodha huyo wa zamani wa Simba kupewa kazi ya kukinoa kikosi cha vijana chini ya miaka 17, mabosi wa JKT Tanzania wamekuwa wakimshawishi arejee uwanjani na wanaamini bado ana uwezo mkubwa.

"Tunamhitaji Bocco, katika tathmini yetu tumegundua hapa Tanzania huwezi kumpata straika kama yeye, japo ana umri mkubwa, lakini ana uwezo kuliko washambuliaji wengi vijana tulionao. Shida yetu kubwa msimu uliopita ilikuwa ni straika.

Tukiangalia hatuwezi kusajili straika wa kigeni, wa hapa ndiyo hawa msimu mzima ana mabao matano tu, tukaona bora twende kwa Bocco ambaye kwa misimu yote aliyocheza Ligi Kuu, alikuwa akipiga mabao yasiyopungua 10, tumeona tumrudishe uwanjani," alisema mtoa habari wetu.

Kiliongeza chanzo hicho kwa sasa wapo katika hatua za mwisho za mazungumzo huku wakiwa wanasubiria jibu chanya kutoka kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Azam FC.

"Mambo yanakwenda vizuri, tuko katika hatua za mwisho kabisa, baada ya hapo tutamtambulisha kama mchezaji na nahodha wa kikosi chetu, tutampa mkataba wa mwaka mmoja, kama akifanya vyema mpaka nusu msimu, tunamwongeza tena mwaka mmoja," kilisema chanzo hicho.

Bocco aliyeichezea Simba kwa misimu saba kuanzia mwaka 2017, alikuwa mchezaji wa kwanza kutangazwa kuachwa na Wekundu wa Msimbazi lakini akiwa amepewa jukumu jipya klabuni hapo.



Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Lameck Nyambaya (katikati), akionyesha tuzo ya heshima aliyopewa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, kutokana na mchango wake wa kukuza na kuendeleza soka nchini. Tuzo hiyo imetolewa na Chama cha Soka Mkoa wa Mtwara (MTWAREFA). **PICHA: DRFA**

# Asma mwenyekiti mpya Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

ASMA Hassan amechaguliwa kwa kura zote kuwa mwenyekiti mpya wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Mkoa wa Dodoma (DOWEFA), katika uchaguzi uliofanyika jijini humo jana.

Nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa imekwenda kwa Debora Mwenda wakati Hilda Masanche na Sakina Mhando wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya DOWEFA.

**Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Asma alisema kuwa anaamini chini ya uongozi wake soka la wanawake Dodoma litazidi kukua.**

"Nitashirikisha na kamati yangu pamoja na Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa (DOREFA), kuhakikisha ligi za wanawake zinachezwa kuanzia ngazi ya chini, tunataka kuongeza ushiriki wa timu katika Ligi Kuu ya Wanawake, tutataka kuipa heshima na hadhi ya juu mkoa wetu wa Dodoma kupitia soka la wanawake," Asma alisema.

Mwenyekiti wa DOREFA, Mohamed Aden, aliwapongeza viongozi wote waliochaguliwa na kuwataka wadumishe umoja ili kutekeleza vyema majukumu yao.

"Ushirikiano na umoja ndio utawapeleka katika kufikia malengo, tunahitaji kuona Dodoma inapata heshima kupitia wanawake, tunaamini na tunauwezo wa kufanya makubwa," Aden alisema.

## Simba yaifunika Orlando Pirates

INATOKA UK. 24

wa, timu hii lazima tuijenge upya, watu wamechoka, wanataka furaha, wanataka makombe, hawataki kuendelea kuyaona ya zamani, wanataka kuyaona mapya, huwezi kuyapata kama hujatengeneza timu bora," meneja huyo alisema.

Ingawa hakuwa tayari kutaja majina ya wachezaji waliokuja nchini kujiunga na Simba, chanzo chetu kimebaini yuko kiungo mshambuliaji, Jean Ohoua (22), kutoka Stella Adjame ya Ivory Coast, kiungo mkabaji mwenye asili ya Angola, Debora Fernandes Mavambo (Mutondo Stars - Zambia), na beki wa kushoto, Valentin Nouma ambaye ni raia wa Burkina Faso na msimu uliopita alikuwa akiichezea Rahimo FC.

Pia yupo winga mchachari, Jushua Mutale, kutoka Power Dynamos ya Zambia.

Kuhusu kuchelewa kutoa 'thank you' kwa wachezaji wengine, Ahmed alisema kinachokwamisha mchakato huo ni baadhi yao bado wana mikataba na kinachofanyika ni mazungumzo ya kuvunja mikataba hiyo.

"Tuko katika mazungumzo ili tuachane nao kwa amani, hatutaki kuwa wadaiwa sugu wa FIFA, tukishamalizana tutamalizia kutangaza tunaowaacha, huku tukisubiri usajili wote ukamilike ndiyo tuanze kutangaza, hatutaki tutangaze leo halafu kesho tukae kimya," aliongeza.

Tayari Simba imeshatangaza itasafiri kwenda katika jiji la Ismailia, Misri ili kuweka kambi kwa lengo la kujiandaa na msimu mpya wa mashindano huku Tamasha la Simba Day likipangwa kufanyika Agosti 3, mwaka huu.


## Gamondi awaita nyota mawindoni

INATOKA UK. 24

fursa hii kuwaambia Wana-Yanga wawe tayari kuanzia tarehe moja tutaanza kutoa taarifa za usajili, wachezaji wetu wapya na wale tunaowaongezea mikataba na tutakaowaacha," Hersi alisema.

Yanga inatarajia kuweka kambi yake Ulaya lakini imeweka wazi imepokea mwaliko wa kucheza mechi za kirafiki za kimataifa katika nchi za Kenya na Afrika Kusini.

Mabingwa hao pia walitangaza watacheza dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini katika kilele cha Siku ya Mwananchi.



Klabu hiyo pia imefanikiwa kuwabakisha nyota wake nyota waliokuwa wanatakiwa na klabu za nje ya Tanzania akiwamo Stephane Aziz Ki, Maxi Nzengeli, Pacome Zouzoua na Djigui Diarra.

# Michezo

Jumapili Juni 30, 2024

Nipashe




Kocha Brazil amvulia 'kofia' Vinícius Júnior

UK. 21



Wachezaji wa Hispania wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya hatua ya 16 Bora ya mashindano ya Euro 2024 dhidi ya Georgia itakayochezwa leo nchini Ujerumani. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAIFUNIKA ORLANDO PIRATES

## ●●● Yamnasa Okejepha, majembe mengine sita yako nchini ili...

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

WAKATI uongozi wa Simba ukithibitisha nyota saba wa kigeni wako nchini kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kujiunda na Wekundu wa Msimbazi, straika wa Rivers United, Augustine Okejepha, amekamilisha mazungumzo ya kuitumikia klabu hiyo katika msimu ujao wa mashindano, imefahamika.

**Taarifa za ndani kutoka Simba zinasema nyota huyo raia wa Ghana amesaini mkataba wa miaka mitatu na anatarajiwa kuwasili nchini mapema wiki ijayo.**

Chanzo hicho kilisema Okejepha ameichagua Simba kutokana na rekodi walizonazo na kukataa dau la Dola za Marekani 220,000 zilizowekwa na mabosi wa Orlando Pirates inayoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini.

"Tunashukuru mchakato wetu wa usajili unakaribia kufika mwisho, idadi kubwa ya wachezaji tuliowalenga wameshapatikana, tunataka kwenda kuanza kambi tukiwa na kikosi kamili," kilisema chanzo chetu.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili wachezaji hao wametua kwa nyakati tofauti kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo na hatimaye kusaini mikataba na kuanza kuitumikia Simba.

Ahmed alisema uongozi wa klabu hiyo umejipanga kufanya usajili mkubwa kwa sababu wanataka kurudisha heshima na hadhi ya klabu.

"Tuna wachezaji wapya saba wa kigeni wapo hapa hapa Tanzania kwa ajili ya usajili, bahati nzuri si watu wengi wanaowafahamu, lakini pia wapo chini ya ulinzi mkali, napenda kuwaambia wanachama na mashabiki wa Simba wasione kimya wakadhani hakuna kinachofanyika.

Wakati haya majembe saba yapo Dar, baadhi ya viongozi wetu wamegawana majukumu, kuna mmoja yuko Zambia, yupo aliyekwenda Ivory Coast, kuna anayesafiri kwenda DRC (Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo), mmoja Maylasia, kote huko wanakwenda kumalizana na wachezaji," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa mara ya kwanza baada ya misimu mingi Simba itakuwa na wachezaji wengi wapya katika kikosi chake na hii inafanyika kwa malengo ya kutengeneza timu mpya itakayorudisha heshima ya klabu.

"Tunafanya ukarabati mkub-

INAENDELEA UK 23

## Gamondi awaita nyota mawindoni

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanatarajia kuingia kambini kesho kwa ajili ya kuanza mazoezi kuelekea msimu mpya wa mashindano wa mwaka 2024/2025.

Wito huo umetolewa na Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ambaye bado yuko kwao alikokwenda kwa ajili ya mapumziko baada ya kumaliza msimu uliopita.

Taarifa kutoka Yanga zinasema Gamondi amewataka wachezaji wote wapya na wale waliosalia katika kikosi hicho kuwapo jijini Dar es Salaam Julai Mosi tayari kuanza kambi.

Chanzo hicho kilisema Gamondi ametuma ujumbe wa simu kwa viongozi, kuhakikisha wanamaliza mchakato wa usajili haraka huku akiwataka wachezaji wote kuripoti kambini kuanzia Julai Mosi, mwaka huu ili kuanza mawindo.

"Kocha ametuma ujumbe, amesema bila kujali mchezaji mpya au wa zamani, pamoja na watu wa benchi la ufundi kila mmoja anatakiwa awe amewasili kambini Julai Mosi, kwa hiyo viongozi wameambiwa wamalize kila kitu kuhusu usajili ili akifika isiwe tena kuna mchezaji hajafika au kukamilisha usajili," kilisema chanzo chetu.

Naye Rais wa Yanga, Hersi Said, amesema klabu hiyo itaanza kutangaza nyota wapya waliosajiliwa na inaowatema kuanzia kesho.

Hersi alisema usajili wa kikosi chao umeshakamilika na kinachosubiriwa ni kukabidhi majina katika Idara ya Habari ya klabu hiyo.

"Tumeshasajili karibu asilima 99, kazi imekwisha, hivi sasa tumeiachia tu Idara ya Habari kutengeneza njia nzuri ya kutambulisha wachezaji, kuna maeneo ambayo tumelazimika kuyaboresha katika kikosi chetu ili kuwa bora zaidi, kwa hiyo nichukue

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >